UKURASA WA 5
**Wafa** katika shimo la choo wakiondoa mbao za ujenzi



UKURASA WA 5
**Atiwa** mbaroni tuhuma kuua mke na mtoto



UKURASA WA 8
HATI FUNGANI MPYA YA NMB
**Programu** ya Sh. Tril 1/- yazinduliwa ikiweka rekodi Kusini mwa Sahara

MID WEEK JACKPOT!
TZS. 718,345,550
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Nipashe
Jumanne Septemba 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581445
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US



Rais CWT, Leah Ulaya

# Fukuto latanda uhai wa CWT

• **Polisi** yawazingira, baada ya rukhsa rais wao anena 'tusi-ingiliwe', wakubaliana kukopa bil. 4/- kununua fulana...*Uk.2*



Baadhi ya wajumbe wa Baraza Kuu la Chama cha Walimu Taifa wakiwa katika kikao jana jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**UKWELI ANAYEDAIWA KUFAULU DARAJA LA I, JINA LAKE KUUZWA**
UTATA umelighubika tukio la mwanafunzi wa kidato cha tano, anayedai...

UKURASA WA 5
**MWINYI ASHANGAA FURSA YA SOKO LA Z'BAR KUTOTUMIWA**
RAIS Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar ina fursa nyingi za...

## Tril. 6.7/- zaibua mageuzi lukuki Sekta ya Afya

UKURASA 4



## Hatimaye mradi wa Dege NSSF wapata mwekezaji

UK. 3

**MICHEZO** YANGA YATAJA JEURI YAO KWA AL MERRIKH UK.24

**KATUNI** UK.6




Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu (katikati), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa NMB, Dk. Edwin Mhede (kulia), wakizindua NMB Jamii Bond jijini Dar es Salaam jana. **Habari Uk.8** **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Fukuto latanda uhai CWT

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KIKAO cha Baraza la Dharura la Chama cha Walimu Tanzania (CWT) jana kilichelewa kuanza kwa zaidi ya saa moja baada polisi kuwazuia wajumbe kuingia ndani ya ofisi ya makao makuu ya chama hicho jijini Dodoma, hadi watakapopata taarifa kutoka kwa uongozi.

Nipashe ilishuhudia 'vutanikuvute' iliyodumu kwa saa moja na dakika 20 na kuchelewesha kikao kilichokuwa kianze saa tatu asubuhi, lakini hadi saa 4.20 asubuhi wajumbe walikuwa nje ya geti huku polisi wakitanda getini, wakiongozwa na Mkuu wa Kituo cha Polisi Dodoma Mjini, Joram Samson.

Polisi hawakuweka wazi sababu za kuzuiliwa wajumbe hao huku baadhi wakidai wameambiwa na aliyekiitisha kikao hicho (Katibu wa CWT, Japhet Maganga) hana mamlaka kutokana na mwajiri wake kumtaka kurudi kufundisha.

Mwalimu Mahanya Kiola, alisema ameshangazwa na kitendo hicho cha kuzuiliwa na polisi kwa kuwa kikao hicho ni cha kupitisha matumizi ya fedha kwa shughuli za chama.

"Hawa polisi tumewauliza 'hili zuio limetoka wapi?', wanasema wamepewa maelekezo kutoka juu, 'kwa nani?' hawasemi. Tunashindwa kuelewa, lazima ifike hatua tuzingatie taratibu, juzi tumekodi ukumbi St. Gasper tumekusanyika pale tunataka kufanya mambo yetu tunazuiliwa na msajili, sababu anayoitoa haina msingi wowote.

"Msajili, yeye jukumu lake ni kuangalia katiba imekiukwa wapi na hakuna sehemu yoyote inayoonesha kipengele hiki cha katiba kimevunjwa, Maganga hustahili, tunamwuliza msajili unapata wapi nguvu hiyo?," alilalamika.

Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Mkinga, James Bulege, alisema chama hakina mgogoro na walimu wala wanachama isipokuwa kuna baadhi ya viongozi wa serikali wanakiharibu kwa maslahi yao.

Alisema, chama cha wafanyakazi ni huru na kikao hicho ni cha dharura kwa mujibu wa katiba na kanuni wamekuja kuzungumza mambo ya chama, lakini wanashangaa kukuta askari polisi getini.

"Leo askari anakuja kuzuia kikao cha chama huru na tumeitwa kuja kukifanya kwa kupata barua kutoka CWT Taifa kama mamlaka inavyosema na tumeombewa ruhusa, lakini askari wamezuia kikao, wanajua tunakuja kuzungumza nini? Hawa tuliowaondosha ndani ya chama tumetumia katiba,"alisema.

Katibu wa CWT kutoka Dar es Salaam, Nassoro Mwinshehe, alisema ameomba nyaraka za amri ya kuwazuia, akajibiwa na polisi kuwa ni amri ya mdomo.

"Sisi ni chama huru cha wafanyakazi, utaratibu wa kuomba kibali ni miaka mitatu, mimi ninajiuliza katika ile barua ukishaomba ukapewa mkataba wa miaka mitatu ikikaribia kuisha unaomba tena na barua inakwambia wakati unataka kurudi itategemea kama nafasi zipo wengi wameendelea kuomba na kupewa, sioni sababu za yeye kuzuiliwa kibali chake.

"Katibu Mkuu ameondolewa kwenye malipo ya mshahara, haiwezekani, kuna 'link', unaomba kwa Katibu Mkuu Utumishi, lakini unaona tangazo kwenye mitandao ya kijamii kuna kudhoofisha vyama vya wafanyakazi," alilalamika.

Baadaye Mkuu wa Kituo cha Polisi Dodoma Mjini, Joram Samson, alitangaza kuruhusu kikao hicho, akisisitiza polisi wanachohitaji ni amani.

"Tunaomba kikao kiendelee kwa amani na sisi tunaondoka kwenda kutekeleza majukumu mengine," alisema.

**RAIS CWT**

Akifungua kikao hicho, Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema ili kuitwa 'mtu wa chama cha wafanyakazi', ni lazima kupitia changamoto na misukosuko.

"Tunapokutana na vitu kama hivi tunaimarika na kujifunza zaidi namna ya kuishi kama wanaharakati wa vyama vya wafanyakazi. Ninawapongeza kwa namna mmekuwa wavumilivu, ingeweza kutokea ramsha lakini mmetumia hekima za kiualimu na ukomavu wa kivyama vya wafanyakazi, mnatulia na kumsikiliza kiongozi wenu wa juu anasema nini.

"Mmeonesha utulivu hadi huko nilipotokea wamesema hakika CWT inajua chama cha wafanyakazi kinatakiwa kiweje. Kuna wakati tunahitaji kufanya kazi kwa maridhiano, kukaa mezani na kufanya kazi pamoja na serikali na vyombo vinavyotusimamia, lakini kuna wakati wa kusimama kama viongozi wa vyama vya wafanyakazi.

"Wakati huo ni sasa, hatuna wakati mwingine wa kusimama kama viongozi wa vyama vya wafanyakazi wakati huu ni sasa na ni leo, hatuna wakati mwingine, tunapaswa kushikamana ili kuwa imara zaidi, hatuna muda wa kupoteza, tuna muda wa kusimama na kuonesha kuwa sisi ni chama cha wafanyakazi,"alisema.

Rais huyo alisema wanafanya shughuli zao bila kuvunja katiba ya nchi na wanatambua na kuheshimu mamlaka, lakini mamlaka lazima itambue na kuheshimu kuwapo vyama vya wafanyakazi.

"Kikao hiki ni halali, uhalali wa kikao hiki uko kwenye katiba na kanuni, tuna ziko mezani kwa msajili wa vyama na huyu msajili anamwakilisha Rais kwenye dawati lake na mara nyingi hatutegemei zitokee ramsha za serikali kwenye chama cha wafanyakazi kinachofanya kazi kwa uhuru wake," alisema.

Kiongozi huyo alisema 'wanazishi' kanuni za Shirika la Kazi Duniani (ILO) na serikali inapaswa kujua kuna uhuru wa vyama vya wafanyakazi kukutana mahali popote na wakati wowote na kufanya kazi zao mahali popote bila kuzuiliwa wala kuingiliwa na chombo chochote cha serikali, isipokuwa kama kuna jambo la msingi kufanya hivyo.

Aliwataka viongozi wa CWT kuwa imara kwenye maeneo yao ili kufuata taratibu zao na kufanya yale wanayotakiwa kufanya bila kuingilia uhuru wa serikali.

"Tutasimama na tutasonga mbele tutahakikisha wale walimu waliotupa nafasi hizi tutawasimamia vizuri na watakuwa na amani kwamba tunafanya kazi tuliyotumwa," alisema.

Aliahidi wako tayari kufanya kazi na serikali na wakati wowote katika shughuli zozote za serikali na kuomba serikali ilinde uhuru wa vyama hivyo.

"Tuweke kumbukumbu kwamba kuna watu walikisimamisha chama kilichotaka kuzama, kilisimama na kuwa imara zaidi. Kikao kinaendelea na kama kuna mtu alitamani sasa tunafanya.

"Hatuoni sababu vikao vyetu vikasimamiwa na polisi, kuna wakati tunasimamiwa kwa sababu mshikamano tumeachana nao, sasa turudi njia kuu, sisi ni wamoja na kama kuna miongoni mwetu anaona haoni sababu ya kuendelea nasi kwa sababu watu fulani hawapo, anaweza akanyoosha mkono wakati huu, si wakati wa kubembelezana," alisema.

## ...Wakubaliana kukopa bil. 4/-

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAJUMBE wa Baraza la Dharura la Chama cha Walimu Tanzania (CWT), jana waliazimia masuala mbalimbali ikiwamo kukopa Sh. bilioni nne kwa ajili ya kununua tisheti na kofia.

Pia wameazimia kuunda kamati ya kuchunguza kwa kina fedha zilizokopwa na kutolewa kwa ajili ya mkono wa kwaheri kwa walimu wastaafu kuanzia mwaka 2015 hadi 2023 kutokana na baadhi ya viongozi wa CWT kwenye mikoa kuonesha shaka kwa wanufaika.

Kikao hicho cha baraza kiliketi jana jijini hapa chini ya Rais wa CWT, Leah Ulaya na viongozi wote wa juu wa chama hicho.

Katika kikao hicho ambacho kilikuwa na ajenda moja ya masuala mbalimbali ya chama yenye vipengele sita, ukiwamo ununuzi wa tisheti kwa ajili ya mwaka 2024, wajumbe waliazimia kupitisha kiwango hicho cha mkopo.

Hata hivyo, haikuwekwa wazi watakapokopa fedha hizo. Vipengele vingine ni mkono wa kwaheri, wazo la kuwa na SACCOS na ujenzi wa makao makuu.

Katika kipengele cha mkono wa kwa heri, Katibu wa CWT, Japhet Maganga, alisema chama kimeanza kutoa mkono wa kwaheri kwa wastaafu 3,459 wa mwaka 2021 na 2022 ambao kila mmoja atapewa Sh. 340,000.

"Kama mtakumbuka ndugu wajumbe kwenye mkutano mkuu mwaka jana tuliazimia kurudisha mkono wa kwaheri baada ya kusitishwa kwa muda, na hawa tuliowapa ndio hawana mkanganyiko, tumeona tuanze nao, wale wengine waliobaki tutawahakiki na kuwapatia mkono wa kwaheri," alisema.

Baada ya taarifa hiyo, wajumbe walitaka kujua kama fedha zilizokopwa kwa nyakati tofauti kwa madai kuwa wanawalipa wastaafu, ni vyema kujua waliolipwa ili kuondoa sintofahamu zinazojitokeza.

"Ninaomba kama ofisi ya Katibu Mkuu ikatupa majibu ya kuridhisha kwamba Sh. bilioni 1.1 wastaafu wote waliolipwa ili tuondoke na orodha hiyo, lakini kama haina baraza hili, linaweza kuunda kamati ndogo ya kuchunguza jambo hili," alisema mjumbe kutoka Mbeya.

Katibu Maganga alisema mwaka 2021 walijaza mkopo wa kukopa Sh. bilioni 1.1 kwa ajili ya kuwalipa wastaafu mkono wa kwaheri na orodha za walimu waliolipwa zipo kwenye Ofisi za CWT mikoa.

Mmoja wa wajumbe kutoka mkoani Kilimanjaro, alisema alipokea orodha ya wastaafu 500 waliolipwa, lakini kulikuwa na majina matatu tu ya wastaafu wa mkoa huo na hajui mengine ni ya wapi.

Rais wa CWT, Ulaya alisema yeyote aliyepelekewa majina ya wastaafu ambayo sio yenyewe yaliyonufaika na mkono wa kwaheri, atoe ushirikiano kwa kamati.

**WAJIONGEZEA POSHO**

Katibu Maganga aliwajulisha wajumbe kuwa kuna ongezeko la fedha wanazopokea kila mwezi Sh. milioni 100 kuanzia mwezi Agosti mwaka huu na kuomba baraza liridhie zitumike kuongeza posho za vikao kuanzia wilaya, Mkoa na Taifa ambapo kwa kauli moja wajumbe walikubali hoja hiyo.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu (CWT), Maganga, alisema hajapewa barua ya kukataliwa kwa ombi lake la kuendelea kuazimwa na chama hicho.

Septemba 23, 2023 lilionekana tangazo lililotolewa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke likimtaka Maganga kurejea katika kituo chake cha kazi.

Katika tangazo hilo, inaonesha Maganga aliomba kibali cha kuazimwa na CWT kwa mara ya kwanza Agosti 2017 kilichomalizika Setemba 30, 2020. Aliomba nyongeza ya kibali cha kuazimwa Juni Mosi mwaka 2020 na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi alimpa nyongeza Agosti 10, 2020 kinachoishia Septemba 30, 2023.

Tangazo linasema Maganga aliomba tena kibali cha kuazimwa mara ya tatu, lakini Katibu Mkuu Utumishi hajaridhia maombi hayo, hivyo mwalimu huyo anapaswa kurejea katika kituo chake cha kazi mara moja Oktoba Mosi mwaka huu.

Nipashe ilimtafuta Maganga ambaye alikuwa kwenye kikao cha baraza la dharura la CWT Taifa jana, alisema "sijapata barua, nikipata nitazungumza, lakini kwa sasa sina cha kuzungumza."

Katibu huyo alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CWT Desemba mwaka jana na mkutano mkuu wa chama hicho kuchukua nafasi ya Deus Seif ambaye kwa wakati huo alikuwa amehukumiwa kifungo cha miezi sita jela baada ya kupatikana na hatia ya kutumia madaraka yao vibaya.

Januari 25 mwaka huu, Maganga na Rais wa CWT, Leah Ulaya waliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa wakuu wa wilaya, lakini hawakwenda kuapa.

Leah aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita wakati Maganga akiteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera.

HABARI KITAIFA

## Adai eneo lake kuvamiwa na CCM

**Na Kulwa Mzee**

MKAZI wa Mbagala Kibonde Maji, Sudi Mohammedi Mnazi, amedai eneo lake kuvamiwa na CCM Tawi la Mchikichini na kushauri kama wanalihitaji wakubaliane walinunue badala ya kulichukua kwa nguvu.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Ardhi la Kata ya Kibonde Maji, Mnazi alisema yeye ni mwanachama wa CCM tangu chama cha TANU, eneo hilo alikuwa akiishi na wazazi wake.

"Nimezaliwa mwaka 1954, nyumba tumepata miaka mingi, tulikuwa tukiishi na wazazi, pembeni kulikuwa na maji yameweka shimo, tulikuwa tunalifukia na eneo hili ni letu.

"Ninachojua CCM wamekuja mwaka huu kuvamia eneo letu na kusema ni lao baada ya kufukuzwa eneo walilokuwa wamepanga kama ofisi.

"Mimi mwenyewe mwanachama wa CCM tangu TANU, CCM juu haina shida, shida iko huku chini, wanataka kutumia mambo yao ya miaka ya nyuma, wanavamia wanachukua eneo, sasa hivi mambo yamebadilika kama wanataka eneo watupe hela tuwauzie," alisema Sudi.

Katibu wa CCM Tawi la Mchikichini, Nyelembe Yunus akizungumzia kiwanja hicho, alisema eneo ni la chama hakikuwa kikifuatiliwa na kwamba lilikuwa chini ya chama miaka 20 iliyopita, lakini hawana hati ndio wanaifuatilia.

Mjumbe wa shina namba 9, Mosi Juma, alisema ni mjumbe miaka minne nyuma, alianza mume wake, ni mwanachama wa CCM, lakini hajawahi kusikia kama eneo hilo ni la CCM.

Katibu wa Baraza la Ardhi, Kata ya Kibonde Maji, Abdallah Kassim baada ya kusikiliza shauri hilo, alisema kasitisha uamuzi kwa muda mpaka jirani aonyeshe mipaka yake, kwa sababu hati walizotoa CCM na hati alizotoa mwenye eneo zinakinzana.

Kassim alisema atatoa uamuzi mpaka atakapoitisha kikao kingine cha Baraza la Kata.




Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, akiwasilisha mada katika kikao kazi kilichoandaliwa na Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na NSSF kilichohudhuriwa na wahariri pamoja na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hatimaye mradi wa Dege NSSF wapata mwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umesema umepata mteja wa kununua mradi wa nyumba za Dege Eco Village, Kigamboni, jijini Dar es Salaam wenye eneo la ekari 302 kwa thamani ya Dola za Marekani 220 (sawa na Sh. bilioni 450).

Aidha, NSSF imesema thamani ya mradi huo wa nyumba 3,750 zilizokuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi ni Sh. bilioni 330 na kwa kuuzwa kwa kiasi hicho, Mfuko utapata faida iliyotarajiwa.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema mradi huo ulikuwa wa nyumba 7,450, lakini hazikukamilika na wako kwenye hatua za mwisho na mnunuzi.

Alisema mradi huo umeuzwa kama ulivyo, ikiwa ni utekelezaji wa uamuzi wa Bodi ya Mfuko na serikali, ili kurudisha fedha za wanachama zilizowekezwa awali katika mradi huo.

"Kwa sasa Mfuko kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali unakamilisha taratibu za zabuni baada ya kukamilika kwa hatua ya tathmini ya zabuni na maafikiano ya bei. Matarajio ni kusainiwa kwa mkataba wa mauzo ya mradi huu kabla ya Oktoba 31, 2023," alifafanua.

Mradi wa Dege Eco ulitakiwa kuanza mwaka wa fedha 2013/2014, lakini ulianza Juni mwaka 2019 na miaka michache usilimama.

**MIRADI MINGINE ILIYOSIMAMA**

NSSF inatekeleza miradi mitano ya nyumba za makazi za Dungu, Toangoma, Mtoni Kijichi, jengo la kibiashara na makazi la Mzizima Towers na hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano, Mwanza.

"Changamoto na kasoro za kizabuni na kimikataba zilizokuwapo zilipelekea miradi hii kusimama mwaka 2016. Miradi hii imepitia hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanyiwa mapitio (review) na ukaguzi maalum ikiwapo ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), iliyokamilika mwishoni mwa mwaka 2020," alisema.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kuanzia Machi mosi, mwaka 2021, Mfuko ulitatua changamoto zilizokuwapo na kuanza utekelezaji wa miradi yote na inatarajiwa kukamilika kati ya Juni na Septemba, mwakani.

**UZALISHAJI SUKARI**

Mashomba alisema mradi wa kiwanda cha sukari Mbigiri wilaya ya Kilosa, unamilikiwa kwa ubia kati ya NSSF asilimia 96 na Jeshi la Magereza asilimia nne katika shamba leye ukubwa wa hekta 4,856 (ekari 12,000) na kiwanda kinatarajiwa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka huku gharama zilizojumuisha ardhi zikiwa ni Sh. bilioni 344.47.

Alisema hadi Juni 30, mwaka huu, utekelezaji wa mradi kwenye mashamba ya miwa ulikuwa ni asilimia 86 na kiwanda asilimia 93 na kwamba asilimia 88 ya gharama zimeshatumika na utakamilika mwishoni mwa Oktoba, mwaka huu.

"Mradi huu utaongeza mapato ya Mfuko, uzalishaji wa sukari nchini, mapato ya kodi wa serikali na kuongeza ajira zipatazo 11,315," alisema.

**KUJIUNGA NA NISS**

Alisema NSSF imefanya mapitio ya mpango wa utoaji wa huduma za Hifadhi ya Jamii katika sekta isiyo rasmi 'National Informal Sector Social Security' (NISS), na kwamba ni kutokana na mpango huo kukosa mafao na huduma zinazowavutia wananchi walio katika sekta isiyo rasmi kujiunga na mfuko.

**MICHANGO YA WANACHAMA**

Mashomba alisema wanachama wanaochangia wameongezeka kwa asilimia 26 kutoka 945,029, Juni 30, mwaka 2021 hadi 1,189,222 Juni mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la wanachama 547,882.

Mkurugenzi Mshomba alisema makusanyo ya michango ya mwezi yameongezeka kutoka Sh. bilioni 97.67 ilivyofika Machi mosi, 2021 hadi kufikia bilioni 143.05, Juni 30 mwaka huu.

Alisema makusanyo ya michango kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 43 hadi kufikia Sh. trilioni 1.718 katika mwaka ulioishia Juni 30 mwaka huu, ikilinganishwa na Sh. trilioni 1.201 zilizokusanywa mwaka ulioishia Juni 30, mwaka 2021.

Kuhusu uwekezaji wa Mfuko, alisema uliongezeka kwa asilimia 111 kutoka Sh. trilioni 3.395, Machi mosi, 2021 hadi Sh, trilioni 7,153, Juni 30, mwaka huu na kwamba kumechangiwa na kukua kwa thamani ya vitega uchumi, michango ya wanachama na mapato ya uwekezaji.

Kwa mujibu wa Mshomba, thamani ya vitega uchumi vya Mfuko imekua kwa asilimia 55 hadi kufikia Sh. trilioni 7.153, Juni 30, mwaka huu kutoka Sh. trilioni 4.622 zilizofikiwa Juni 30, 2021.

Mshomba alisema wastani wa mapato ya uwekezaji kwa mwezi hadi Juni mwaka huu yalifika Sh. bilioni 72.06, ikiwa ni ongezeko la asilimia 92 ikilinganishwa na Sh. bilioni 37.35 zilizokusanywa Machi mwaka 2021.

**ULIPAJI MAFAO**

Kuhusu mapato halisi, alisema yameongezeka kutoka wastani wa asilimia 3.31, Machi mwaka 2021, hadi kufikia asilimia 5.32, Juni mwaka huu, huku mapato ya uwekezaji kwa mwaka yakiogezeka kwa asilimia 93 na kufikia bilioni 864.76 kutoka bilioni 448.17 kipindi hicho.

Kwa upande wa mafao, NSSF imelipa zaidi ya Sh. bilioni 61.93 kwa mwezi kama mafao kwa wanufaika mbalimbali ikiwa ni ongezeko la asilimia 22 ikilinganishwa na Sh. bilioni 50.58 zilizolipwa kwa mwezi kipindi kilichoishia Machi mosi, 2021.

# Wizara yajipanga utafiti uchimbaji madini, kuachana na kubahatisha

**Na Pilly Kigome,** GEITA

WIZARA ya Madini imejipanga kufanya utafiti wa kijiolojia uchimbaji wa madini 2030 nchi nzima kwa ajili ya utambuzi wa maeneo sahihi yenye madini na kuachana na uchimbaji wa kubahatisha.

Mpango huo wa serikali utaanza kununua mitambo 15 ya uchorongaji wa miamba kwa ajili ya utafiti wa kina wa madini na utafiti huo utakaoanza Mkoa wa Geita.

Waziri wa Madini, Antony Mavunde, alisema hayo katika semina elekezi kwa wachimbaji wadogo na wakubwa, mkoani Geita.

Waziri Mavunde alibainisha mkakati huo wenye jina 'VISION 2030 Madini ni Maisha na Utajiri' kuwa serikali imejipanga kufanya utafiti wa madini nchi nzima kwa lengo la kupata taarifa zitakazoweza kufungamanisha sekta ya madini na nyingine za kiuchumi.

Alisema hali ya utafiti wa madini mpaka sasa umefanyika kwa asilimia 16 pekee ambazo taarifa zake zinatumika na serikali lengo lake ni kuongeza taarifa kupitia utafiti utakaofanywa na GST.

Mpaka sasa sekta ya madini inachangia asilimia 56 ya fedha za kigeni kwa asilimia 9.1 ya Pato la Taifa (GDP).

"Imebaki miaka saba tu mpango huu uweze kukamilika Watanzania waweze kuneemeka," alisema.

Alisema sekta ya madini mwaka wa fedha uliopita iliingiza asilimia 56 ya mauzo yote nje ya nchi kwa bidhaa za madini na kupata Dola bilioni 3.3 sawa na zaidi ya shilingi trilioni saba.

Alibainisha na kwa upande wa Pato la Taifa madini lilichangia asilimia 9.8 na kwenye pato la kodi za ndani sekta ya madini iliingiza asilimia 15 sawa na Shilingi trilioni mbili pato la ndani kwa mwaka wa fedha uliopita.




# Tril. 6.7/- zaibua mageuzi lukuki Sekta ya Afya

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya imeeleza namna Sh. trilioni 6.7 zilizotengwa na serikali kwa ajili ya sekta ya Afya katika uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, zilivyoibua mageuzi makubwa katika sekta hiyo.

Katika mkutano wa wahariri na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alitaja mafanikio hayo yanajumuisha uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na kuongeza ujuzi katika rasilimali watu iliyoko katika sekta hiyo.

Alisema, serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wananchi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya karibu na maeneo yao kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa, ukijumuisha ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya maeneo mbalimbali nchini.

Dk. Mollel alikumbusha kuwa serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya Afya; mwaka 2021/22 ikitenga Sh. trilioni 2.1, mwaka 2022/23 ikatenga Sh/ trilioni 2.2 na mwaka huu 2023/24 imetenga Sh. trilioni 2.4.

Aliyataja maeneo yaliyopewa kipaumbele katika uwekezaji huo kuwa ni miundombinu ya utoaji huduma za afya, huduma za uchunguzi wa magonjwa, upatikanaji bidhaa za afya, kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa ubobezi na mfumo wa ugharamiaji huduma za afya.

Dk. Mollel, akifafanua mikakati iliyowekwa katika kuimarisha miundombinu ya utoaji huduma za afya, alisema katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi mwaka huu, vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezwa hadi kufikia 11,040 kulinganishwa na vituo 8,549 mwaka 2021.

Kati yake, hospitali zilikuwa 430, vituo vya afya 1,030 na zahanati 7,458, kliniki 906 na maabara binafsi 1,216.

"Serikali imeendelea kukamilisha hospitali za rufani za mikoa katika mikoa mipya ya Njombe, Songwe, Geita, SImiyu na Katavi. Awamu ya kwanza ya ujenzi huo imekamilika na tayari hospitali zote zimeanza kutoa huduma.

"Vilevile, serikali imeendelea kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini Mtwara na Hospitali ya Kanda Chato ambapo tayari huduma zimeanza kutolewa," alibainisha.

Alisema serikali pia imeimarisha miundombinu ya kutolea huduma za dharura nchini kwa kujenga majengo ya huduma za dharura (EMD) 128 katika hospitali za ngazi ya taifa, maalum, kanda na mkoa, na kuziwekea vifaa na vifaa tiba hadi Machi mwaka huu na ICU 73 zimejengwa na kukamilika.

"Kuimarika kwa huduma hizi kumewezesha hospitali kuokoa maisha ya wagonjwa wanaohitaji huduma hizo kwa asilimia 20 hadi 40. Uwekezaji huu katika miradi ya maendeleo umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 891.5," alisema.

Kuhusu huduma za uchunguzi, Dk. Mollel alisema serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa katika eneo hilo, mashine za MRI saba, CT-Scan 32, na X-ray za kisasa 199 na Angio-Suite moja inayowezesha kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu, zimenunuliwa.

Alisema uwekezaji huo umewezesha nchi kuwa na jumla ya MRI 13, CT-Scan 45 na X-ray za kisasa (digital X-ray) 543.

Kuhusu upatikanaji bidhaa za afya, Dk. Mollel alisema serikali imeendelea kuwekeza katika upatakaji dawa, jumla ya Sh. bilioni 442 zikitolewa katika uongozi wa Rais Samia.

Naibu Waziri huyo pia alisema serikali imeendelea kuimarisha huduma za kibingwa nchini kwa kuweka utaratibu mzuri wa kusomesha watumishi.

**BIMA YA AFYA**

Dk. Mollel alitumia muda mwingi katika mkutano huo kusisitiza umuhimu wa Watanzania wengi zaidi kujiunga na huduma ya bima ya afya ili kuchangiana katika matibabu na hivyo kuifanya mifuko husika kuwa endelevu.

Alisema serikali imekuwa inafanya marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya ili kuruhusu makundi ya wananchi kujiunga kwa hiari.

Alisema takwimu zinaonesha hadi kufikia Juni mwaka huu, wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) walikuwa 4,821,233 sawa na asilimia nane ya wananchi wote milioni 61.7.

Alizitaja changamoto zinazokwaza ujumuishaji wa wananchi katika mfumo wa bima ni pamoja na uhiari wa kujiunga kwa makundi hayo kwa kuwa wengi hujiunga wakiwa tayari ni wagonjwa.

"Mwaka 2016, NHIF ilianzisha mpango kwa watoto walio chini ya miaka 18, maarufu Toto Afya Kadi kwa lengo la kuwezesha kundi hilo kwa ujumla wake kujiunga na bima kupitia shule za awali, msingi na sekondari ili kunufaika na huduma za afya.

"Hata hivyo pamoja na uhamasishaji uliofanywa kwa kipindi cha miaka saba, bado mwitikio haukuwa wa kuridhisha kwani idadi ya watoto walioji-andikisha ilikuwa 210,000 kati ya lengo la watoto milioni 25 kwa kipindi hicho.

"Vilevile, kupitia kundi hilo asilimia 99 ya watoto walioandikishwa walikuwa tayari na matatizo ya kiafya. Sh. bilioni tano zilizokusanywa kama michango yao, lakini Sh. bilioni zilitumika kugharamia matibabu yao.

"Hali hii ni kinyume cha dhana na misingi ya uendeshaji wa mfumo wa bima ya afya. Ili mfumo wa bima ya afya uwe endelevu, ni lazima kila kundi lin aloandikishwa liwe na uwezo wa kuchangiana gharama za matibabu," alifafanua.

Dk. Mollel alisema katika kutatua changamoto zilizopo, serikali inamilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inayolenga kuimarisha Mfumo wa Bima ya Afya nchini kwa kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanajiunga na utaratibu huo kulinganishwa na hali ilivyo sasa.

# Ukweli anayedaiwa kupata Daraja la I kidato cha IV, jina lake kuuzwa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

UTATA umelighubika tukio la mwanafunzi wa kidato cha tano, anayedai kuwa na jina la Sifika Daniel Ruben na kuchaguliwa kujiunga na masomo ya Sayansi katika tahasusi ya Fizikia, Kemia na Hesabu (PCM), Shule ya Sekondari ya kitaifa ya Namwai, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro aliyedai kushindwa kwenda shule kwa kukosa ada na kuamua kwenda kutafuta kazi za ndani.

Tukio hilo limezua gumzo mitandaoni, baada ya shule husika kudai anawahadaa Watanzania ili atumie jina hilo ambalo si lake.

Wakati utata huo na matokeo yake ya mitihani ya NECTA yakizua gumzo katika mitandao ya kijamii, jina lake halisi linaelezwa kuwa ni Sifael Tawel Elirehema.

Tukio hilo limemwibua Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Malaamu, Dk. Dorothy Gwajima, ambaye ameandika kwenye kundi songezi, kuwa ametuma maofisa jamii kumhoji binti (anayedai kuchaguliwa) na pia anawasiliana na Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, kwa hatua zaidi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Namwai, Anna Urassa, mwanafunzi halali mwenye sifa zote za kujiunga na tahasusi hiyo, Sifika Daniel Ruben, alishapokewa shuleni hapo Agosti 13, mwaka huu na kuanza masomo yake ya Sayansi.

"Ukweli ni kwamba shule yetu tulimpokea mwanafunzi anaitwa Sifika Daniel Ruben tarehe 13/8/2023 akitokea Shule ya Sekondari ya Mkombozi. Mtoto huyu alifaulu kwa ufaulu wa divisheni one ya pointi 10 (daraja la kwanza), na kwa sasa yuko darasani anaendelea na masomo.

"Ila tarehe 30/8/2023 aliripoti mwanafunzi mwingine kwa jina hilo hilo la Sifika Daniel Ruben.

...Huyo mwanafunzi (anayedai) hakuwa na result slip (cheti chenye matokeo), wala hakuwa na Leaving Certificate. Mwanafunzi halali ambaye ni Sifika Daniel Ruben, aliyeko darasani alikuwa na vielelezo vyote.

Ili kujiridhisha na utata huo, Mkuu huyo wa shule, alimtaka mlezi aliyefika shuleni hapo na mwanafunzi anayejiita Sifika Daniel Ruben, aliyejiandikisha katika rejesta ya wageni, tarehe 30/8/2023 kama Janeth J. Temba, mkazi wa Arusha (Moshono), afuatilie result slip shuleni alikomaliza kidato cha nne.

Lakini, kabla ya kuondoka alipata wazo la kutafuta namba ya simu ya Mkuu wa Sekondari ya Mkombozi ili kupata taarifa za mwanafunzi huyo.

"Baada ya kufanya naye mawasiliano na kumpiga picha mwanafunzi huyo wa pili mwenye jina hilo hilo la Sifika Daniel Ruben, alimdhihirishia kwamba aliyeko kwenye picha, haitwi Sifika Daniel Ruben, bali anaitwa Sifael Tawel Elirehema.

Alimwambia alikuwa anasoma masomo ya Arts (Sanaa) na alipata Divisheni Zero (daraja la sifuri)."

Nipashe ilipofika katika shule hiyo iliyoko West Kilimanjaro, kilomita saba kutoka mji mdogo wa Sanya Juu, ilizungumza na mwanafunzi Sifika Daniel Ruben, ambaye anaelezwa kuwa na vielelezo vyote vinavyomruhusu kujiunga na masomo hayo ya PCM.

"Mimi niliripoti hapa shuleni (Namwai) tarehe 13/8/2023 na nikaruhusiwa kuendelea na masomo, lakini baadaye alikuja mwanafunzi ambaye alisema anaitwa Sifika Daniel Ruben.

Alisema, mwanafunzi huyo anaitwa Sifael Tawel Elirehema. "Tulisoma naye sekondari (Mkombozi) lakini yeye alikuwa akichukua masomo ya Arts na mimi nilikuwa nikichukua masomo ya Sayansi."

"Mimi ndiye Sifika Daniel Ruben, namba yangu ya mtihani ni S 0850/0136 na ndiye niliyepata Divisheni One ya pointi 10.

Mlezi wa mwanafunzi anayedaiwa kujitolea kumfadhili mwanafunzi anayedai kudhulumiwa haki yake, Janeth Temba, mkazi wa Arusha (Moshono), aliiambia Nipashe kuwa, alimpeleka mwanafunzi huyo shuleni na gharama zote kuanzia sare, viatu, vitabu na kila kitu alimnunulia.

Alisema mtoto huyo alipokewa na Makamu Mkuu wa shule na kuambiwa ataje namba ya mtihani, lakini alivyotaja, akaulizwa "mbona namba hiyo inafanana na mwanafunzi ambaye tayari ameshapokewa? Mtoto akajibu hapana."

Alisema, Sifika Daniel Ruben aliyekuwa tayari darasani aliitwa na wote wakaambiwa waandike matokeo yao yalivyokuwa.

"Alikuja kwangu kama dada wa kazi nyumbani, akanieleza kwamba amefaulu ila wazazi wameshindwa kumlipia ada, mama yake ni mgonjwa na baba yake hana uwezo wa kumlipia mahitaji ya shule.

...Nikajichanga mimi na mume wangu, tukanunua vitabu na hivyo vitu vingine tukampeleka shule. Nilipompeleka shule situation (hali) niliyokutana nayo ndio kama hiyo."

Alisema, alipoona utata unazidi, aliamua kumpigia mama wa mtoto huyo na kumwomba amtumie majina matatu ya mtoto wake na alimtumia hilo la Sifael Tawel Elirehema. "Hivi mzazi wake anaweza kudanganya jina la mwanawe?"

**MAMA SIFIKA**

Alipotafutwa kuzungumzia utata kuhusu madai hayo, Zuhura Athuman, ambaye ni mama wa mtoto huyo, alisema mwanawe Sifael Tawel Elirehema, aliwahi kumweleza kwamba alifaulu, lakini hakumwambia kwa kiwango gani.

"Huyu mtoto (Sifael Tawel Elirehema) anayesemekana ni Sifika Daniel Ruben, wakati anafanya mtihani, mimi sikuwa naye, nilikuwa mgonjwa.

"Aliwahi kuniambia amefaulu, lakini kwenye kufuatilia sikuweza kwa maana mimi ni mgonjwa, niko kwetu najiuguza nilipata presha ya macho."

## Jafo aagiza kampuni za madini kuzingatia utunzaji wa mazingira

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo ameziagiza kampuni zote nchini zinazojihusisha na uchimbaji madini kuzingatia taratibu na sheria zinazohusiana na mazingira ili kuisaidia Tanzania na dunia kukabiliana na janga la mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, ameshauri kampuni hizo kwenda kujifunza namna Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) inavyotekeleza Sera ya Utunzaji wa Mazingira kwa kuwa ndio kampuni mfano inayochimba madini na kuzingatia sheria hiyo.

Jafo alitoa maagizo hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kupanda miti na kutembelea mabanda ya Maonesho ya Sita ya Teknolojia ya Madini yanayoendelea katika Uwanja wa Bombambili, mjini Geita.

"Kampuni ambayo inajitahidi kuhifadhi mazingira ni GGML. Kwahiyo, ninapenda kuwatia moyo kwamba muendelee na ari hiyohiyo kuhakikisha mazingira yanatunzwa.

"Kama tutakuza uchumi kupitia madini, lakini tusipotunza mazingira, tutapa madhara makubwa. Kumbukeni mabadiliko ya tabianchi ni janga duniani. Hakuna taifa ambalo lipo salama kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kiwango cha joto kinaongezeka kila kukicha.

"Tuendelee kukuza uchumi, lakini tulinde mazingira. GGML mmeendelea kuwa wadau wakubwa na sisi serikali tunahitaji wadau kama ninyi ili kushirikiana kuhakikisha nchi inasonga mbele," alisema.

Awali akitoa salamu za Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela, Mkuu wa Wilaya ya Nyang'wale, Grace Kingalame, alisema kwa mwaka huu mkoa umepanga kupanda miti 1,500.

Alisema kuwa tangu kampeni ya upandaji miti ianze, mkoa huo umekuwa kinara katika hilo na kufanikisha kupanda miti zaidi ya milioni moja.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema atasimamia sekta hiyo kuhakikisha shughuli zote za uchimbaji zinaendana na sera ya utunzaji mazingira.

Meneja Mazingira wa GGML, Mhando Yusuph alisema mgodi huo umeweka sera ya utunzaji mazingira ambayo inagusa maeneo makubwa matatu.

Alitaja maeneo hayo ambayo ni kuzuia uchafuzi wa mazingira, kufuata sheria zinazohusu mazingira na kufanya maboresho endelevu katika suala la mazingira.

"Kwahiyo, kila kitu kinachofanyika ndani ya mgodi kinazingatia utunzaji mazingira. Tunazingatia usimamizi wa mazingira ndani ya mgodi kwa shughuli zote za uchimbaji na kuhakikisha hatuchafui vyanzo vya maji kama mito na mabwawa yaliyo ndani ya mgodi.

"Pia katika kuhakikisha sera hii inazingatiwa, huwa tunafanya upimaji wa maji yaliyomo ndani ya mgodi. Kwa kuwa uchimbaji unahusisha kuondoa rasilimali za miti kunapotokea eneo halitumiki tena huwa tunapanda miti," alisema Yusuph.

# Mbaroni tuhuma kuua mke, mtoto

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia mwanamume mkazi wa Kijiji cha Kaloleni, wilayani Songwe (jina linahifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi) kwa tuhuma za mauaji ya Editha Msokwa (38) na mtoto wake mchanga wa miezi sita, Esther Emanuel.

Chanzo cha mauaji hayo kinadaiwa ni wivu wa mapenzi baada ya mtuhumiwa huyo kumtuhumu mkewe huyo kuzaa mtoto nje ya ndoa.

Mtuhumiwa huyo ambaye kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya Mwambani, wilayani Songwe baada ya kujeruhiwa na wananchi, anadaiwa kumvizia mkewe akiwa amelala usiku na mtoto wake huyo wa miezi sita na kuwanyonga kabla ya kuuburuta mwili wa mkewe huyo na kwenda kuuficha katika kibanda nje ya nyumba yao.

Akithibitisha kushikiliwa kwa mtuhumiwa huyo, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Rashid Ngonyani, alisema jana kuwa kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa Septemba 24 mwaka huu.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa baada ya kuokolewa na viongozi wa kijiji chini ya Mwenyekiti Laiton Waya kutoka katika kundi la wananchi wenye hasira kali waliomkamata baada ya kufanya tukio hilo la mauaji ya kinyama na kuanza kumshushia kipigo.

"Mtuhumiwa huyo kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya Mwambani akiwa chini ya ulinzi, na uchunguzi wa awali wa Jeshi la Polisi unaonesha mtuhumiwa kabla ya kutekeleza mauaji hayo walikuwa na mgogoro na mkewe kwa kumtuhumu kuzaa nje ya ndoa," alisema Kaimu Kamanda Ngonyani.

Alisema kuwa jeshi hilo linaendelea na uchunguzi na pindi utakapokamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.



Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Switbert Mkama, akisikiliza maelezo kuhusu mradi wa lambo katika Kijiji cha Melela Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro alipofanya ziara ya kukagua Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi ashangaa fursa ya soko Z'bar kutotumiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar ina fursa nyingi za masoko ya bidhaa za wajasiriamali kutokana na kuwapo hoteli nyingi za kitalii, hatahivyo haijatumiwa ipasavyo.

Alisema, ni vyema wadau wakashirikiana ili wajasiriamali wazalishe kulingana na mahitaji na viwango vinavyohitajika na kunufaika na fursa za soko katika sekta ya utalii.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa tamasha la kuadhimisha mwaka mmoja wa kuanza kazi kwa wakala wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, visiwani humo.

Alisema juhudi za kuwawezesha wananchi lazima zijikite katika upatikanaji wa masoko ndani na nje ya nchi.

"Nazitaka taasisi zote zinazohusiana na usimamizi wa sekta ya utalii kuhakikisha wajasiriamali wetu ndiyo wanufaika wa kwanza wa fursa zinazopatikana katika sekta hii ili kupunguza uzalishaji wa bidhaa tunazozalisha kutoka nje ya nchi na kuimarisha soko la ndani kwa wajasiriamali wetu," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema, serikali inathamini juhudi zinazochukuliwa na wananchi wanaojiajiri katika shughuli za ujasiriamali na kuthamini michango ya sekta za fedha kuwasaidia wajasiriamali kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao.

Alisema serikali imejizatiti kutimiza malengo ya ilani ya CCM ya mwaka 2020/2025 ya kuzalisha ajira 300,000 kwa kipindi cha miaka mitano na fursa nyingi zitatokana pia na kuwawezesha wananchi kujiajiri na wajibu wa serikali ni kuandaa mazingira wezeshi.

"Natoa wito tuendelee kubuni na kusimamia vyema utekelezaji wa mikakati na mipango mizuri ili wananchi wa Zanzibar kuzibaini na kuzitumia fursa hizo," alisema Dk. Mwinyi.

Kadhalika, serikali inaendelea na kuimarisha miundombinu na mazingira ya kufanya biashara ikiwamo masoko na maendeleo ya kufanya biashara katika vituo vya daladala lengo likiwa ni kuwapatia wakala wengi wa bidhaa zao wajasiriamali katika maeneo hayo ambayo kuna mkusanyiko mkubwa wa watu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Mudrick Ramadhan Soraga, alisema wizara yake kupitia wakala wa uwezeshaji wataendelea kutoa mikopo isiyo na riba na kutoa elimu ili kuwafikia wajasiriamali wote kwa Unguja na Pemba.

Mkurugenzi Mtendaji wa wakala wananchi kiuchumi, Juma Burhani alisema, katika utekelezaji wa shughuli zake, Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar imechukua juhudi za kuwezesha wajasiriamali kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili ili kukua na kujenga uchumi shirikishi.

Alisema miongononi mwa juhudi zilizochukuliwa katika kuweka mazingira mazuri ni pamoja na kuwaunganisha wajasiriamali kuingia katika makubaliano na taasisi zinazotoa fursa zinazowahusu kwa kuwapatia mitaji, mafunzo na kuwatafutia masoko ya bidhaa zao kwa lengo la kuwajengea uwezo na kupata masoko rafiki ya bidhaa ndani na nje ya nchi.

"Hadi kufikia leo hii jumla ya Sh. 20,232,616,514.80 (Unguja 12,333,420,608 na Pemba 7,899,195,906) zimetolewa kwa wanufaika 19,373 (sawa na ongezeko la asilimia 155) ambapo 7,527 ni wanaume na 11,846 ni wanawake, kupitia CRDB tumeshakusanya marejesho 7,595,264,572.50," alisema.

Aidha, alisema Wakala imeweza kutanua wigo wake wa utoaji wa mikopo kwa kuwa na mikopo inayotokana asilimia kumi ya makusanyo ya ndani ya Serikali za Mitaa hadi sasa shilingi bilioni 1.7 zimekusanywa na wakala tayari ishapeleka fomu kwa halmashauri ya wilaya Kusini na Micheweni ili kuanza kutowa mikopo hiyo.

# Watatu wafa katika shimo la choo wakiondoa mbao

**Na Jenesta Jasson,** BUKOBA

WATU watatu ambao ni mafundi ujenzi katika Kijiji cha Katoma, Halmashauri ya Wilaya Bukoba mkoani Kagera, wamefariki dunia huku mmoja akinusurika kifo wakati wakimalizia shughuli za ujenzi wa shimo la choo.

Tukio hilo lilitokea juzi baada ya mafundi hao kuingia ndani ya shimo la choo kwa ajili ya kuchukua vipande vya mbao vilivyobaki ndani ya shimo hilo wakati wa ujenzi wake.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Emmanuel Katalaiya alisema jana kuwa mafundi hao waliingia katika shimo hilo wakifuatana kwa ajili ya kusaidiana kutoka ndani ya shimo hilo, lakini walifikwa na umauti kutokana na kukosa hewa.

Ofisa Habari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Kagera, Sajenti Shabani Mussa, aliyefika eneo la tukio, alitaja waliofikwa na umauti kufuatia ajali hiyo ni Denis Philbert (40), Ayoub Benjamini (35) na Fabius Babiligi (30), wote mafundi ujenzi. Sababu ya vifo vyao ni kukosa hewa shimoni.

"Baada ya kuwatoa shimoni, tuliwakimbiza katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera ambako watatu walibainika kuwa wamefariki dunia," alifafanua Sajenti Mussa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Dk. Mseleta Nyakiroto, alisema walipokea miili ya watu hao waliopoteza maisha katika tukio hilo. Miili yao imehifadhiwa hospitalini huko.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NSSF inavyolinda usalama wa maisha ya wastaafu kwa mafao

**WANACHAMA** wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), waliostaafu kazi, wana uhakika wa kuishi maisha bila wasiwasi kutokana na mafao wanayolipwa kupitia michango yao waliyowekeza kwenye mfuko huo.

Umuhimu wa mfanyakazi kujiunga na mfuko huo, licha ya kulipwa pesa ya mkupuo wakati anapostaafu, lakini analipwa mafao yake kila mwezi mpaka mwisho wa maisha yake.

Baadhi ya watu wanapofikia muda wa kustaafu na kutokuwa na akiba inayomwezesha kuendesha maisha yake, huishia kuishi maisha duni na wengine kutochukua muda mrefu na kufariki dunia kutokana na msongo wa mawazo.

NSSF katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, mwaka huu, ililipa Sh. bilioni 61.93 kwa mwezi kama mafao kwa wanufaika mbalimbali ikiwa ni ongezeko la asilimia 22 ikilinganishwa na Sh. bilioni 50.58 zilizolipwa kwa mwezi kipindi kilichoishia Machi 1, 2021.

Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa madai ya fao la upotevu wa ajira (unemployment benefit) na mkupuo maalum (special lumpsum).

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, wanufaika wa mfuko wanalipwa mafao yao kuliko fedha waliyowekeza.

Mfuko huo umehakikisha kuwekeza katika miradi mbalimbali ili uweze kumudu kuwalipa wanachama wake na kuondoa malalamiko.

Malipo ya mwaka ya mafao kwa wanufaika mbalimbali wa mfuko yaliongezeka kwa asilimia 25 na

kufikia Sh. bilioni 743.17 katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023 ikilinganishwa na Sh. Bilioni 594.33 zilizolipwa katika mwaka wa fedha ulioshia Juni 30, 2021.

Mfuko umefanya maboresho mbalimbali ya mifumo ya utendaji kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Baadhi ya maboresho yaliyofanyika ni kuanzishwa kwa mfumo wa kujihudumia kwa ajili ya Waajiri (Employer Portal), Mfumo wa kujihudumia kwa ajili ya Wanachama (Member Portal) pamoja na mfumo wa ukaguzi wa wanachama (Inspector Portal).

NSSF imeendelea kuimarisha mifumo na usimamizi wa fedha ili kuepuka mianya ya upotevu wa fedha, kuendelea kumudu gharama za uendeshaji pamoja na kulipa mafao stahiki kwa wastaafu na wanufaika wengine.

Kwa mujibu wa taarifa za ukaguzi, mfuko umekuwa ukipata Hati Safi (unqualified reports) kutokana na kaguzi zilizofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hati safi za mkaguzi zinathibitisha kuwa fedha za wanachama zipo salama.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF amewahakikishia wanachama kuwa mfuko huo umejiwekea malengo ya kumfanya mtu anapofikia muda wake wa kustaafu, kwa mfano amepeleka vielelezo vyote vinavyotakiwa, basi siku inayofuata mafao yake yawe yameshaandaliwa.


Mfuko kwa sasa unajitahidi kulipa mafao wanachama wake muda usiozidi siku 30 tangu walipopeleka vielelezo vyote vinavyohitajika kulipa mafao.

Utaratibu huu unasaidia kuondoa usumbufu kwa wanachama na kuwawezesha kupata mafao yao kwa wakati na kuwawezesha kupanga mipango yao kwa muda waliojipangia.

Jambo la muhimu kwa wanachama ni kufuatilia kwa waajiri wao kama michango yao inawasilishwa kwa wakati ili wanapofikia muda wa kustaafu wasipate usumbufu wa kurudishwa kufuatilia michango yao.

Vilevile, wanachama wanashauriwa wanapoacha kazi sehemu moja na kupata nyingine michango yao waiendeleze ili ukifika muda wa kustaafu wapate kikokotoo kizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Udanganyifu huu ni mzigo kwa taifa

**KUWAPO** kwa udanganyifu katika mitihani kwenye baadhi ya shule za msingi na sekondari, linaweza kuwa ni janga linaloshindikana kupatiwa ufumbuzi , lakini kibaya zaidi ni kulibebesha taifa mzigo wa kusomesha na kugharamia mafunzo kwa wanafunzi wanaodanganya na wasio na uwezo.

Kuendelea kujitokeza matukio ya udanganyifu huo kila mitihani inapofanyika, licha ya kwamba maonyo yalishatolewa kunaonyesha jinsi watu wanavyopenda kubebesha mzigo mkubwa nchi wakati hawastahili.

Kwa mfano mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka huu unaomalizika mwezi huu umekutana na majanga ikielezwa kuwa baadhi ya walimu na wanafunzi wa sekondari, wamenaswa wakiwafanyia mtihani watahiniwa wa darasa la saba.

Tukio hilo limetokea hivi karibuni mkoani Mwanza, likathibitishwa na Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Wilbroad Mutafungwa.

Ikumbukwe kuwa matukio ya wizi au udanganyifu katika mitihani yamekuwa yakijirudia kila mwaka, kana kwamba ni jambo la kawaida, licha ya shule kadhaa kufutiwa matokeo, wahusika kushitakiwa na hata kuadhibiwa kisheria.

Kila mwenye ufahamu awe mwanafunzi , mzazi, mlezi au mwalimu anajua kuwa ni vibaya kuiba mitihani, lakini kwa nini inakuwa ni rahisi hivyo? Lengo lake ni nini? Ninadhani umefika wakati sasa serikali kuchukua hatua kali zaidi ikibidi kutunga sheria ambazo zinaweza kumaliza tatizo hilo ambalo madhara yake ni makubwa kwa sasa na baadaye.

Madhara hayo ni pamoja na kutumia fedha nyingi kusomesha mbumbumbu na kuwaacha wenye stahili, kukosa wataalam wa fani mbalimbali wenye sifa zinazotakiwa kufanyakazi serikalini na hata katika mashirika ya umma na binafsi.

Sidhani kama mzazi au mlezi anayemtakia mema mtoto wake anaweza kukubali udanganyifu wa aina hiyo.

Kushiriki udanganyifu huo ni kukosa uaminifu, ni vyema kurudi kwenye maadili mema na kuwasaidia watoto wasijihusishe na vitendo hivyo ambavyo ni kikwazo katika maendeleo yao ya kielimu na taifa pia.

Kutofanya maandalizi kabla ya mitihani kunaweza kuwa sababu mojawapo ya kuwafanya baadhi ya wanafunzi washiriki katika vitendo vya udanganyifu huo.

Kufanya udanganyifu ili mwanafunzi apate alama ambazo hazilingani na uwezo wake darasani, ni sawa na kuandaa wasomi feki wa baadaye. Hivyo, ninadhani ipo haja kwa kila mdau wa elimu kushirikiana na serikali kwa kupaza sauti kupinga vitendo hivyo.

Iwapo kila mdau wa elimu atapaza sauti ya kupinga vitendo hivyo, udanganyifu huo hautaonekana kama jambo la kawaida, badala yake utakemewa kila kona.

Hivyo, ni vyema wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wakapewa hamasa ya kujisomea ili wawe na vitu vingi wanavyovielewa, na kujibu vizuri mitihani badala ya kusubiri kutumia mbinu za udanganyifu katika mitihani.

Wanafunzi wasidumaze akili kwa kutojisomea wakitegemea kufaulu kwa njia ya mkato ambayo mwisho wake ni kulifanya taifa kuwa na wasomi ambao hawana msaada kwa nchi yao.

Badala ya kutumia mbinu nyingi za kujipanga kufanya udanganyifu, watenge muda huo kujisomea zaidi ili waweze kujibu mitihani kulingana na jinsi walivyofundishwa.

Ninaamini kuwa kujitahidi kujifunza kama wanavyojitahidi kuiba mtihani, wanaweza kupata alama za juu zinazolingana na uwezo wao wa darasani na sio za udanganyifu.

Ni kweli mwanafunzi anaweza kushawishika kufanya udanganyifu,

lakini ni vyema akaepuka mtego huo wa kimaadili. Aheshimu kile kilichompeleka shule.

Kimsingi, mwanafunzi hana budi kusoma kwa bidii wakati wote na sio kusubiri hadi mtihani ukaribie au kusubiri kufanya udanganyifu ambao mwisho wake si mzuri

Ninaeleza hivyo, kwa sababu inawezekana wizi au udanganyifu katika mitihani ukamwongoza mtu kwenye matendo mengine makubwa ya udanganyifu anapokuwa mtumishi iwe katika ofisi za umma au za binafsi.

HABARI KITAIFA

# Wateja warahisishiwa huduma kukata bima popote

**Na Zuwena Shame**

SHIRIKA la Bima Zanzibar (ZIC) limerahisisha upatikanaji wa huduma kwa kumuwezesha mteja kukata bima muda wowote akiwa popote nchini.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZIC, Arafat Ally Haji, alisema Shirika limekuja na ubunifu kwa kuanzisha ZIC Bima App huduma itayowasaidia wateja kukata bima wakiwa sehemu yoyote na muda wowote.

Aidha, Shirika limeanzisha bima mahsusi kwa wateja wake wa kike ikiwa na lengo la kuunga mkono jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali zote mbili kuwapa kipaumbele katika shughuli za kijamii na kimaendeleo.

Arafat, alifafanua kuwa bima hiyo ni kwa ajili ya wanawake wanaomiliki vyombo vya moto lengo ni kumkinga dhidi ya majanga ya moto, ajali, wizi wa gari au hata vipuli na hasara itakayosababishwa na mteja kwa watumiaji wa barabara pamoja na mali zao.

Pia, Shirika linawahudumia wateja wake wanaosafiri na kuwapa kinga wakiwa nje ya nchi muda wote wa safari zao kupitia huduma yake ya Bima ya safari.

Alisema bima ya safari inampa kinga msafiri popote nchini na nje ya nchi dhidi ya majanga kama kupotea kwa hati ya kusafiria, dharura ya kiafya safarini, kughairishwa kwa safari, kupotea kwa mizigo na vilevile gharama za kurudisha mwili.

"Huwezi kufanikiwa bila ya kuwa na ushirikiano thabiti na wadau wengine katika soko, Shirika la Bima la Zanzibar linafanya kazi na washirika tofauti ili kuimarisha huduma zetu, pia tunashirikiana Reinsurers ili kuongeza uwezo wetu wa kuhimili ulipaji wa madai yanapotokea," alisema.

"Kwa kushirikiana na benki tumerahisisha njia za ulipaji wa ada za bima kwa kushirikiana na benki kupitia mikopo ya ada za bima ijulikanayo kama Insurance Premium Funding (IPF), zinazomuwezesha mteja kufanya malipo ya bima kwa awamu na kwa riba nafuu, kwa sasa Shirika lina makubaliano na benki zaidi ya 11 katika kurahisisha upatikanaji wa mikopo hiyo kwa wateja wetu," alisema.

Kadhalika, alisema kwa kutambua mchango wa mitandao ya simu katika kuendeleza mafanikio ya Shirika la Bima la Zanzibar kwa kushirikiana na mitandao hiyo Shirika limeweza kurahisisha upatikanaji wa huduma ya bima kupitia simu za kiganjani na kuongeza kasi ya ufikiwaji wa wateja wa bima nchini kote.

**"Huwezi kufanikiwa bila ya kuwa na ushirikiano thabiti na wadau wengine katika soko, Shirika la Bima la Zanzibar linafanya kazi na washirika tofauti ili kuimarisha huduma zetu, pia tunashirikiana Reinsurers ili kuongeza uwezo wetu wa kuhimili ulipaji wa madai yanapotokea," alisema.**



Vijana wa mji wa Sirari mkoani Mara wakiokoa baadhi ya bidhaa zilizokuwa kwenye lori lenye namba T 366 DCN kushika moto. Gari hilo lilikuwa limebeba mali hizo kutoka nchini Kenya juzi. **PICHA: SAMSON CHACHA**

# Serikali kujenga mradi kuvuta maji Ziwa Victoria wa bil. 42/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali imepanga kujenga mradi wa maji wa Sh. bilioni 42 kwa ajili ya kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria na kuyasambaza kwenye kata sita za Wilaya ya Muleba.

"Kwa kuanzia, serikali imetoa Sh. milioni 800 kwa ajili ya kuyavuta kutoka ziwani, yaje kwenye tangi lililojengwa ili yasafishwe na yatibiwe kisha tuyasambaze kwenda vijijini. Tumeshafanya hivyo kwenye miji ya Tarime, Musoma Vijijini na sasa tumeanza Bunda, Busega, Magu na Geita. Kote huko tunatoa maji ziwani na kuleta vijijini," alisema.

Aliyasema hayo juzi wakati akiwahutubia wakazi wa mji wa Muleba kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Fatuma, wilayani humo.

Alizitaja kata hizo kuwa ni Kikuku, Bureza, Kagoma, Muleba, Magata, Kikuku na Gwanseli na kuongeza kuwa utafiti ukikamilika utasaidia kubaini ni vijiji vingapi tupeleke maji. "Tunaposema kata, ni pamoja na vijiji vyake vyote."

Alisema katika sekta ya maji, mbali na Sh. bilioni 42, Februari mwaka huu serikali ilitoa Sh. bilioni 5.73 kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa maji kwenye wilaya hiyo. Akitoa mchanganuo, Waziri Mkuu alisema: "Mradi wa maji Bulamula ulipewa Sh. milioni 681; Rutenge Sh. milioni 600; Ilemera Sh. milioni 599; Katare Sh. bilioni 2.96 na Kyamiyorwa Sh. bilioni 3.2."

Wakati huohuo, Waziri Mkuu, aliwataka wakazi hao wawe wavumilivu wakati serikali ikiendelea kuratibu suala la upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wanaoishi maeneo ya jirani na mipakani.

"Kitambulisho cha Taifa ni usalama wa nchi, ni usalama wa taifa letu; kwahiyo anayestahili kukipata ni Mtanzania tu. Na kujua Kiswahili siyo utanzania. Kwahiyo, inabidi tuwe makini na kila mmoja wetu awe mzalendo na lazima tutambuane," alisisitiza.

Alisema amepokea maoni ya wabunge wa mkoa huo ya kwamba serikali ipeleke maofisa wengi zaidi wa Uhamiaji na NIDA ili wafanye uchunguzi wa waombaji na kuwafanyia uhakiki.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo wilayani Masasi mkoani Mtwara, Hamza Machuma (aliyevaa fulana nyekundu) akimkabidhi funguo ya pikipiki mmoja wa bodaboda kati ya bodaboda 17 aliyewakabidhi pikipiki hizo jana wilayani Masasi ili wajiajiri na kuondokana na umasikini. **PICHA HAMISI NASRI.**

HATI FUNGANI MPYA NMB

# Programu ya trilioni 1/- yazinduliwa ikiweka rekodi Kusini mwa Sahara

## ●Msajili wa Hazina, CMSA wakoshwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua rasmi programu mpya yenye hati fungani zenye thamani ya jumla ya Sh. trilioni moja, huku ikitajwa ya kwanza kwa ukubwa kusini mwa Jangwa la Sahara.

Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna, amesema kwa kuanzia, programu hiyo ya miaka 10, ilianza jana na toleo la kwanza la hati fungani ya Sh. bilioni 75, itakayodumu kwa miaka mitatu, ikipewa jina la Hati Fungani ya Jamii (NMB Jamii Bond).

Kwa mujibu wa Zaipuna, kiasi hicho kilichoanza jana kinaweza kuongezwa kwa Sh. bilioni 25 zaidi kutegemea na mwelekeo wa soko utakaojitokeza.

Zaipuna alibainisha katika uzinduzi rasmi wa programu hiyo jana jijini Dar es Salaam, kuwa fedha zitakazokusanywa zitatumika kutoa mikopo inayolenga nishati mbadala na mazingira katika maeneo kama: kuzuia na udhibiti wa uchafuzi mazingira, usimamizi wa majisafi na majitaka na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Pia itakuwa ni kwa ajili ya mikopo ya kuwawezesha wanawake na usawa wa kijinsia, nyumba nafuu, usalama wa chakula, huduma za afya, elimu na vijana," alibainisha Zaipuna.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu huyo, mbali na Sh. bilioni 75 walioanza kukusanya jana, pia kutakuwa na matoleo mengine katika Programu hiyo ya Muda wa Kati (MTN).

Katika uzinduzi huo jana, Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, alisema serikali inajivunia ubunifu wa viwango vya NMB, huku Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, akitaja Hati Fungani hiyo kuwa ya kwanza kwa ukubwa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Katika uzinduzi huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Zaipuna, alisema benki yake inaanza kuiuza rasmi Jamii Bond kote nchini kuanzia jana Septemba 25 hadi Oktoba 27 mwaka huu na baada ya hapo itapatikana katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kwa wanunuzi watakaoikosa katika kipindi hicho.

"NMB Jamii Bond ni ya kipindi cha miaka mitatu, hadi Novemba 2026, ambako wawekezaji wake watapata riba ya asilimia 9.5 kwa mwaka na italipwa kwa vipindi vinne kwa mwaka. Kiasi cha chini ni Sh. 500,000 na mnunuzi atapaswa kujaza fomu katika matawi na kwa mawakala wa DSE waliopewa kibali na CMSA.

"Wanunuzi wa Hati Fungani hii ni watu wote, binafsi, mashirika na kampuni. Lengo ni kukusanya Sh. bilioni 75, lakini CMSA imeturuhusu kufanya ongezeko (green shoe option) la Sh. bilioni 25. Kwa hiyo, tunaweza kwenda hadi Sh. bilioni 100.

"Tumeruhusiwa na CMSA kuuza Hati Fungani hii kwa shilingi za Kitanzania, lakini kwa Dola za Kimarekani, ambako tumepewa idhini ya mauzo ya Dola milioni 10 na ongezeko la Dola milioni tano, hivyo kufanya mauzo ya Dola kuwa yanayoweza kufikia milioni 15," alisema Zaipuna.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo alisema fedha zitakazopatikana zitatumika kutoa mikopo inayolenga matokeo chanya na endelevu katika jamii, ikiwamo miradi ya nishati mbadala, miradi ya kuzuia na udhibiti wa uchafuzi mazingira, usimamizi wa majisafi na majitaka na miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Pia itakuwa ni kwa ajili ya mikopo ya kuwawezesha wanawake na usawa wa kijinsia, nyumba nafuu, usalama wa chakula, huduma za afya, elimu na vijana," alibainisha Zaipuna.

Alishukuru taasisi zote zilizoshirikiana nao, zikiwamo Benki Kuu ya Tanzania (BoT), CMSA, DSE na ABSA Tanzania ambayo ni Mshauri Mwenza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, Mkama, alishukuru Ofisi ya Msajili Hazina kwa kuzijengea taasisi za fedha mazingira wezeshi katika kukuza uchumi, huku akisema kuwa mnamo Agosti 31 mwaka huu, CMSA ilitoa idhini kwa NMB kutoa Hati Fungani hiyo ambayo ni sehemu ya Programu ya Muda wa Kati yenye thamani ya Sh. trilioni moja.

"CMSA ni taasisi ya serikali yenye jukumu la kuhakikisha hati fungani zinazotolewa zinakidhi matakwa na vigezo vya kisheria. Mnamo Agosti 31, tulitoa idhini kwa NMB kutoa Jamii Bond, ambayo fedha zitakazopatikana zitaelekezwa katika miradi mbalimbaili ya kijamii kwa ustawi wa umma.

"Leo (jana) Septemba 25 tunaiambia dunia kuwa NMB imekidhi matakwa ya kisheria kwa mujibu wa CMSA, jumuiya za kimataifa kiasi cha kupewa idhini ya kuiingiza sokoni Jamii Bond.

"Historia inaandikwa leo, NMB imekuja na bidhaa ya hadhi ya juu, hatujawahi kuwa na Hati Fungani ya thamani kubwa kiasi kisi hiki, hii ni rekodi, sio tu kwa Tanzania na Afrika Mashariki, bali ni kubwa zaidi kuwahi kutolewa na taasisi yoyote iliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema.

Msajili wa Hazina, Mchechu, aliwashukuru washirika wa mchakato huo, hususani wasimamizi BoT, CMSA na DSE kwa walichofanya kufanikisha jambo kubwa na la kihistoria kutokea katika sekta ya fedha nchini. Ni kitu cha kujivunia na kujipongeza.

"Kazi nzuri inayofanywa na NMB, inaipa Ofisi ya Msajili heshima tukiwa ndio wasimamizi wa sekta ya fedha. Sisi kama serikali tunafurahia sana uwekezaji wetu ulioko NMB, tunajivunia na ndio 'model' ambayo tutaitumia na kuingiza katika taasisi na mashirika yetu, kwa sababu tumeiona faida yake.

"Ni jambo jema sana soko linapochagizwa na viongozi imara na wabunifu kama waliopo NMB, kwa kuwa viongozi waliolala wanalinyonya soko. Ukiwa na benki kubwa kama hii, ubunifu unaoona mbali ndio jambo la kujivunia. Hakika mmethubutu kuthibitisha uimara kwa kuzindua 'bond' ya Sh. trilioni moja.

"Menejimenti na wafanyakazi, chini ya Bodi ya Wakurugenzi, mnazitendea haki nafasi zenu, hasa ukizingatia tuna mazingira sahihi, rafiki na ya kweli kukuza ustawi wa sekta ya fedha yaliyowekwa na uongozi wa Rais Samia Hassan Suluhu, ambaye amedhamiria kuleta mageuzi chanya katika sekta hii," alipongeza.

# 'Serikali iajiri wasaidizi wa wanafunzi wenye ulemavu'

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MWALIMU wa elimu maalum katika Shule ya Msingi Chalinze, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani, Mwanahamis Nguzo, ameomba serikali kuangalia uwezekano wa kuajiri wasaidizi wa watoto wenye mahitaji maalum wanapokuwa shuleni.

Nguzo amesema kukosekana wasaidizi kunasababisha walimu kufanya kazi za kuwapa huduma wanafunzi hao na hata kuharibu ratiba ya vipindi wanapohitaji usaidizi katikati ya vipindi vya masomo.

Vilevile, mwalimu huyo ameomba kukamilishwa mahitaji katika bweni la watoto hao ili kupunguza adha ya utoro kwa wanaoishi mbali na shule hiyo ambao wanahitaji msaada wa kuletwa shuleni na wazazi wao kila siku. Baadhi hushindwa kufika shuleni kutokana na gharama za usafiri.

Aliyasema hayo juzi wakati Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Bagamoyo ilipotembelea miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri ya Chalinze. Ilikagua bweni la watoto wenye mahitaji maalum katika shule hiyo.

Mmoja wa wazazi wa watoto wenye mahitaji maalum, Salma Juma, alisema bweni hilo litakamilishwa mahitaji yake na wanafunzi kukaa huko, kutapunguza gharama za usafiri wanazotoa kila siku.

"Gharama za usafiri kwa mwezi makadirio ni Sh. 40,000 kwa mwanafunzi. Sasa kwa mzazi ambaye hana uhakika wa ujira inakuwa vigumu kwake kumudu na hivyo mwanafunzi kuwa mtoro na kukosa vipindi.

"Kukiwa na bweni shuleni, kutasaidia hata wazazi ambao uwezo wao ni mdogo kuwaleta watoto shuleni," alisema.

Mzazi huyo alisisitiza suala la kuwa na wasaidizi kwa kuwa watoto hao ni vigumu kuwaacha wenyewe. Wanapokuwa nyumbani na shuleni wanatakiwa kuwa na watu wa kuwaangalia kwa karibu ili kuzifikia sehemu zote ambazo wanataka kufika kama wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhani Possi, alisema Sh. milioni 80 zimetolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya bweni hilo na tayari limekamilika baada ya halmashauri kuongezea fedha nyingine na hatua inayofuata sasa ni kukamilisha vifaa ili watoto waanze kulitumia.

Katika ziara hiyo, kamati ilitembelea na kukagua miradi yenye thamani ya Sh. bilioni mbili, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Badamoyo, AbdulSharifu Zahoro, akiwakumbusha watendaji kuzingatia uadilifu katika utendaji kazi wao.

**"Gharama za usafiri kwa mwezi makadirio ni Sh. 40,000 kwa mwanafunzi. Sasa kwa mzazi ambaye hana uhakika wa ujira inakuwa vigumu kwake kumudu na hivyo mwanafunzi kuwa mtoro na kukosa vipindi.**



## TBS yafanya ukaguzi bidhaa bandia, yatoa elimu

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limefanya ukaguzi wa kushtukiza wa bidhaa zilizopitwa na wakati na kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi katika Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga.

Ofisa Usalama wa Chakula wa TBS, Kanda ya Kaskazini, Mariam Maarufu, alisema shirika hilo limejipanga kuhakikisha linaondoa bidhaa hafifu sokoni, ikiwemo zilizopitwa na wakati ili kulinda afya za walaji.

Aidha, TBS imelenga kuwapa elimu wananchi hao kuhusu umuhimu wa kuzingatia muda wa matumizi ya bidhaa husika hasa za chakula.

Maarufu, alisema wamebaini na kuziondoa sokoni baadhi ya bidhaa hasa za vinywaji ambazo zimepitwa na wakati na kuwasisitiza wafanyabiashara kuzingatia muda wa matumizi wa bidhaa ikiwemo na kuhakikisha wanauza bidhaa bora

"Katika kijiji cha Msomera, tumefika na kufanya ukaguzi katika maduka kadhaa ambapo tumebaini na kuziondoa sokoni bidhaa ambazo zimepitwa na wakati, lakini pia tumetoa elimu kwa wananchi kuhakikisha wanaangalia muda wa mwisho wa matumizi ya bidhaa kabla ya kuzinunua," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara walipongeza shirika hilo kwa kutoa elimu kwani itawasaidia kutatua changamoto walizokuwa wakikumbana nazo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Msomera, Martine Paraketi, alipongeza TBS kwa kuwakumbuka na kufanya ukaguzi pamoja na kutoa elimu maana imewafumbua mambo mengi hasa kuhusu matumizi ya bidhaa.

## Muheza kuchanja mbwa 2,700, kudhibiti ugonjwa wa kichaa

**Na Steven William** MUHEZA

WILAYA ya Muheza mkoani Tanga imejiwekea lengo la kuchanja mbwa 2,700 kwa mwaka huu, lengo likiwa ni kujikinga dhidi ya ugonjwa wa kichaa.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Mifugo Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Edward Mgaya, katika uzinduzi wa chanjo ya mbwa na paka kiwilaya iliyofanyika katika kiwanja cha Kijiji cha Mkanyageni.

Alisema kuwa katika shughuli hiyo wanalengo la kuchanja mbwa 2,700 wilaya nzima mwaka huu wa 2023 na katika uzinduzi huo wamechanja mbwa 50.

Aliwahimiza wananchi kuendelea kuchanja mbwa wao kila baada ya mwaka ili kuwaepushia tatizo la kupata ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

Akizungumza baada ya kutoa chanjo kwa baadhi ya mbwa walioletwa ili waweze kupatiwa chanjo hiyo alisema ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni hatari sana, unaweza kuambukizwa kwa mbwa ambaye akamuambukiza mwanadamu kwa kumng'ata jambo ambalo linaweza kuhatarisha maisha ya mwanadamu.

Alisema kuwa ili kumtambua mbwa mwenye kichaa ni anapotiririsha mate kutoka mdomoni pamoja kuwa na tabia ya kung'ata kitu chochote anachokiona.

Naye Ofisa Mifugo Mkuu, Zakaria Swai, alisema ni vema wananchi wakawa wanawapeleka mbwa wao kupatiwa chanjo hata kwenye vituo vya afya ili kuweza kuwaepusha kupata maradhi ya kichaa cha mbwa.

# Timu ya ufuatiliaji usafirishaji mafuta kutoka Burundi yawasili

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

TIMU ya kiufundi iliyoundwa na Rais wa Burundi, Evarist Ndayishimiye, kufuatilia mfumo wa usafirishaji wa mafuta kutoka Tanzania kwenda nchini humo, imewasili nchini kwa ajili ya kukutana na kufanya mazungumzo ya kibiashara na kampuni za uagizaji na uingizaji wa mafuta kutoka nchi zinazouza mafuta kwa wingi duniani.

Mazungumzo hayo yanalenga pia kuangalia fursa za kibiashara ili kupata uzoefu na kuwavutia kuwekeza Burundi.

Jana, Mwenyekiti wa timu hiyo, Meja Jenerali, Sibomana Ignce, alisema Burundi imechagua kufanya biashara hiyo na Kampuni ya GBP kwa kuwa wamejiridhisha wana bidhaa za kutosha kukidhi mahitaji ya nchi yao.

Meja Jenerali Ignce, alisema lengo la ujio wao ni kuangalia namna watakavyoweza kuendesha biashara hiyo kutokana na ukaribu wa Kituo cha GBP Tanga.

Alisema "Tumetembelea baadhi ya kampuni za Tanzania na tukaona GBP ya hapa Tanga ina kituo ambacho kipo karibu na Burundi, kuliko vituo vingine vilivyopo Dar es Salaam.

"Lakini pia kuna vitu zaidi, ambapo meli inapofika hapa (Tanga) haichukui muda mrefu kupakua shehena ya mafuta ghafi na magari hayakawii kufika nchini kwetu".

Aliongeza "Kubwa zaidi ni kwamba GBP tuna uhusiano tangu Machi mwaka huu ambapo walisafirisha mafuta kuja Burundi na wametushawishi kwa namna wanavyofanya kazi, tunaamini tunapoelekea tutazidi kudumisha mahusiano kati ya Serikali ya Burundi na Tanzania kupitia GBP".

Mfanyabiashara ya mafuta nchini Burundi, Irakizi Herve, alisema wamefurahishwa na vitu vingi vilivyopo Tanzania, hasa kampuni kubwa za mafuta, ambazo hazilingani na zilizoko nchini mwao.

Zaidi aliongeza: "Tumetembelea vituo vingi, lakini vituo vya GBP, naona wana msimamo mzuri kwa Tanzania, sasa ninaamini kama itatumika vizuri kati ya Burundi na Tanzania kufanya biashara nzuri, uzalishaji wa GBP ni mkubwa na nadhani ndio kampuni kubwa kwa nchi hii kwani ina vituo vikubwa hasa hiki cha Tanga."

Mkurugenzi Mkuu wa GBP -Tanga, Badar Sood, alisema wamefurahishwa na ujio wa timu hiyo kwa ajili ya mapatano ya kibiashara kati yao na taifa hilo.

"Tumefurahi kuona wenzetu wa Serikali ya Burundi wamekuja kufanya biashara na sisi na kikubwa namshukuru sana Rais wetu kwa kudumisha demokrasia na biashara kwani leo hii majirani zetu wamekuja kutaka biashara kwetu kutokana na mazingira mazuri katika nchi yetu,"alisema Sood.



Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Edward Mgaya (mwenye koti jeupe), akimchanja mbwa kwa ajili ya kinga ya ugonjwa wa kichaa juzi katika uzinduzi wa chanjo kiwilaya iliyofanyika Kijiji cha Mkanyageni wilayani hapo, lengo la mwaka huu ni kutoa chanjo kwa mbwa 2,700, juzi wamechanja mbwa 50. Kushoto ni Ofisa Mifugo, Abdallah Franus. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# RC aingilia mgogoro wavuvi, askari Hifadhi ya Ziwa Manyara

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, ameunda timu maalum itakayofanya kazi kwa ajili ya kupata mwarobaini wa mgogoro kati ya wavuvi wa eneo la Mto wa Mbu na askari wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

Mgogoro huo ulisababaisha kifo cha mtu moja, huku wavuvi wengine wawili kutojulikana walipo hadi sasa.

Mei 22 mwaka huu wakati wavuvi wakiendelea na shughuli zao za uvuvi katika Kitogoji cha Magomeni Kijiji cha Jangwani Kata ya Mto wa Mbu walivamiwa na askari wa Hifadhi ya Taifa ya Manyara waliokuwa katika doria hali iliyozua mapigano na kusababisha kifo cha mvuvi mmoja na wengine wawili kupotea ambao hadi sasa hawajulikani walipo.

Akizungumza kwenye mkutano wa hadhara katika Kata ya Mto wa Mbu mwishoni wa wiki , Mongella aliuagiza uongozi wa Kijiji cha Jangwani kuchagua wananchi sita watakaoshirikiana na timu ya wataalam kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Monduli na ofisi yake, ili kupata mwarobaini wa kuweka mpaka kati ya hifadhi na vijiji, vinavyozunguka ziwa hilo kwa upande wa Mkoa wa Arusha.

"Tunaomba muda tuje na majawabu hapa Oktoba mwaka huu yenye mwelekeo kupitia kamati hii, itayofanyia kazi masuala yote ilikiwemo hao wavuvi wawili mnaodai walikamatwa na askari wa hifadhi na mpaka sasa hawajulikani walipo,"alisema.

Aidha, Mongella alisema kamati hiyo pia itafanyia kazi uvuvi wa katori unaotumia makokoro na kuvua kila kitu ziwani, hali ambayo ni hatari kwa mazalia ya samaki na samaki wadogo.

Kuhusu fedha za uvuvi zilizotolewa na TAWA Sh. milioni 35 kwa Kijiji cha Jangwani, Mongella alisimamisha matumizi ya fedha hizo, kutokana na mkutano mkuu wa kijiji kutoshirikishwa matumizi ya fedha hizo, ambapo Sh. milioni 17 zimeshatumika.

Kwa mujibu wa Mongella kamati hiyo, itafanya kazi kwa muda mfupi kadri iwezekanavyo ili Oktoba mwaka huu suluhu ya mpaka kati ya vijiji na hifadhi hiyo iwe imepatikana.

Awali Hamisi Hassan (maarufu Dogo Janja), akizungumza kwa uchungu huku akibubujikwa na machozi mbele ya Mongella alisema wavuvi wa Kijiji cha Jangwani wamekuwa wakifanya kazi za uvuvi kwa hofu kubwa kutokana na askari wa hifadhi wanaofanya doria kuvamia eneo la kijiji ambalo ni sehemu ya ziwa na kuwapiga hali ambayo wakati mwingine inasababaisha vifo.





# H/shauri yakusanya 200,000/- ada ya upimaji wa ardhi mwaka huu

**Na Timothy Itembe,** MARA

MADIWANI wa Halmashauri ya Tarime vijijini, wameilalamikia Idara ya Ardhi katika halmashauri hiyo kutokana na kukusanya ada ya upimaji ardhi chini ya makisio Sh.milioni 89.1 kwa mwaka 2023.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo, Diwani Kata ya Binagi, Marwa Maligiri, alisema idara hiyo imekusanya mapato ya Sh.200,000 pekee kama ada ya upimaji ardhi.

Alisema makisio halisi yalikuwa ni kukusanya zaidi ya Sh.milioni 89.1 kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Solomon Shati, alisema katika mwaka huo wa fedha halmashauri ilitazamia kukusanya Sh. bilioni 44.6 kutoka katika vyanzo mbalimbali, hadi kufikia juni 30, mwaka huu Halmashauri ilikuwa imekusanya Sh.bilioni 43.7 sawa na asilimia 98 ya lengo la mwaka.

Aidha, aliliambia baraza hilo kuwa Halmashauri ya Wilaya Tarime ilipata hati safi ya ukaguzi wa hesabu kwa mwaka 2021-2022 licha ya Idara ya Ardhi kushuka kwa kiasi kikubwa katika ukusanyaji mapato.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Saimon Kiles, aliomba halmashauri kuongeza nguvu katika makusanyo

**Alisema makisio halisi yalikuwa ni kukusanya zaidi ya Sh.milioni 89.1 kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023.**

na kuhakikisha wanatafakari zaidi maeneo yasiyofanya vyema katika ukusanyaji mapato, ikiwa ni pamoja na idara ya ardhi ili kuwawezesha kutekeleza shughuli za kimaendeleo.

"Hatutaki kusikia miradi imekwama kwa sababu fedha za kutekeleza miradi kwa wananchi zipo kinachotakiwa ni kuondoka wote na kwenda kufanya kazi kwa pamoja"alisema Kiles.

Baraza hilo la kupokea taarifa ya utekelezaji shughuli za Halmashauri ya Wilaya yaTarime kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022-2023 liliambatana na uchaguzi wa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ambapo Diwani Petro Ntogoro alichaguliwa kushika nafasi hiyo.




Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, akipata maelezo ya magari kutoka kwa Ofisa Masoko na Mawasiliano wa Kampuni ya Gf Trucks & Equipments Ltd, Smart Deus, alipokagua mabanda ya maonyesho ya madini mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBS: Tutashirikiana na wanahabari wapate taarifa sahihi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAMISAA wa Sensa Tanzania Bara, Anne Makinda, amesema Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari nchini katika kuhakikisha vinapata taarifa sahihi.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa waandishi wa habari wa mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Simiyu juu ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yaliyofanyika mkoani hapa.

Alisema katika kuhakikisha viongozi wa ngazi mbalimbali nchini wanawajibishwa juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, waandishi wa ,habari wanatakiwa kutumia vyema ofisi hiyo kupata taarifa ili kuwahoji vizuri na kupata muafaka sahihi.

Vilevile aliwataka waandishi hao kuhakikisha wanafikisha taarifa za takwimu kwa wananchi, lengo likiwa ni kuwasaidia kuwahoji viongozi wao juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo husussani katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi.

Katika hatua nyingine alieleza kuwa kabla ya Desemba mwaka huu ofisi hiyo itakuwa tayari imetoa taarifa zaidi ya 400 zinazohusu mambo mbalimbali yaliyopatikana katika sensa iliyofanyika mwaka 2022.

"Kupitia taarifa hizo waandishi wa habari pamoja na wananchi wataweza kuwawajibisha viongozi wao juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, aliwakumbusha waandishi wa habari kushiriki kikamilifu katika kuandika na kuwafikishia taarifa wananchi pamoja na serikali juu ya matokeo ya takwimu hizo.

Kadhalika alieleza kuwa serikali imerahisisha utekelezaji wa majukumu na wajibu wake kupitia takwimu zilizopatikana kutokana na Sensa ya Watu na Makazi iliyopita.

"Kwa sasa tunatoa huduma mbalimbali za kijamii kupitia taarifa za sensa kwani kabla ya hapo tulikuwa tukiwasikiliza viongozi wa maeneo husika ambao hata hivyo wengi wao walikuwa wakivutia maendeleo kwao na kusababisha maeneo mengine kukosa huduma,"alieleza Makilagi.

Baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki katika mafunzo hayo waliiomba serikali pamoja na viongozi wa kisiasa kuacha tabia ya kuwaandama pindi wanapotoa takwimu ambazo zimepatikana kupitia maeneo husika.

# DC Kishapu ataja mikakati uimarishaji sekta ya elimu

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkunde amesema mikakati ya uimarishaji wa sekta ya elimu umeendelea kufanyika katika wilaya hiyo, lengo likiwa ni kuondoa adha zilizokuwa zikiwakabili wanafunzi za kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Mkunde alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kueleza kuwa mikakati hiyo imefikiwa baada ya wilaya hiyo kupokea zaidi ya Sh. bilioni 40.4 kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alieleza kuwa licha ya kuzifikia sekta mbalimbali zikiwemo za afya, maji, barabara, kilimo na mifugo kupitia fedha hizo katika sekta ya elimu wamefanikiwa kujenga shule mpya mbili za msingi ambazo ni Winenekeja na Nguzombili.

Alisema kupitia shule hizo wanafunzi wameondokana na hatari ya kushambuliwa na wanyama wakali pindi walipokuwa wanakwenda shuleni.

Inaelezwa kuwa baadhi ya wanafunzi ambao wanaishi katika Kijiji cha Winenekeja Kata ya Igaga wilayani humo ni miongoni mwa waathirika wa mashambulizi ya mara kwa mara ya wanyama aina ya fisi.

Lakini kupitia mkakati wa ujenzi wa shule katika maeneo hayo pamoja na samani umedhibiti adha hiyo.

Alisema: "Bado ipo miradi mingine inayoendelea kutekelezwa kuimarisha sekta hiii niiagize sasa ofisi ya mkurugenzi kwa kushirikiana na wakuu wa idara pamoja na madiwani, kusimamia vizuri fedha za utekelezaji wa miradi hii ya maendeleo na ikamilike kwa wakati na kutoa huduma".

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Winenekeja, Jonas Nkondu, aliwaambia waandishi wa habari waliotembelea kuona shule hiyo kuwa shule hiyo itakuwa msaada mkubwa kwa watoto walioukuwa wakienda shule umbali za zaidi ya kilometa nane.

Alisema katika kuwalinda watoto wao na fisi, walifanya mkutano na suala hilo kulikabidhi kwa Jeshi la Jadi (Sungusungu) ili kuwalinda watoto majira ya alfajiri wanapokwenda shule na majira ya jioni wanaporudi.

Diwani wa Igaga wilayani humo, James Kamoga, aliishukuru serikali kwa kujenga shule hiyo mpya ya msingi katika Kijiji cha Winenekeja ambayo thamani yake ni Sh.milioni 561 na ina madarasa 16 na matundu ya vyoo 24 na itaanza kutoa elimu mwakani.

Zephania DC; anayebadili matatizo visiwani kuwa fursa za kielimu



Ukurasa 12




Ukurasa 13

Usichukie hisabati unaihitaji ukiwa ndani na nje ya darasa



Ukurasa 14

Kuzingatia muda wa kulala, kuamka uleule ni tiba, afya

Nipashe
TESA
Jumanne Septemba 26, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

TEKNOLOJIA

NA CLAUDIA KAYOMBO, SINGIDA

# Ubunifu kuvuna asali ulivyonusuru nyuki, wafugaji na kuokoa misitu

UBUNIFU unaowagusa wananchi moja kwa moja wakiwamo wakulima, wafugaji na wavuvi vijijini ndiyo iliyokuwa ndoto ya mwalimu Catherine Mtani wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) aliyelenga kuwafanyia maajabu wafuga nyuki wanaoteseka wakati wa kuvuna asali.

Catherine wa Idara ya Ushonaji, amebuni vazi mahususi kwa mrina asali linalomkinga asing'atwe na nyuki wakati wa kufungua mizinga na kupakua asali au kuushusha na kuichukua.

Mwalimu Catherine wa Idara ya Ushonaji, amebuni vazi analosema linatengenezwa kwa kitambaa kizito, lastiki, stifu na wavu linalomfunika anayevuna kwa kuanzia nyayoni hadi kichwani wakati wa kuvuna asali .

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe chuoni hapo anasema namna anavyolishona vazi hilo nyuki hawezi kupenya na kuifikia ngozi ya mtu na kumdhuru badala yake linamuweka salama na hata nyuki pia kwa sababu hapati madhara.

Kwa upande mwingine uvunaji wa asali unatumia moto ili kuwachoma na kuwalewesha kwa moshi na joto na kusababisha madhara kama kuchoma misitu, kuharibu mazingira ya asili na mazao mashambani.

"Lakini mfugaji akivaa vazi hili anausogelea mzinga, anarina asali na kuondoka nayo bila kumdhuru nyuki wala yeye binafsi pamoja na mazingira," anasema Mwalimu Catherine.

Mbunifu huyo anaongeza kuwa vazi hilo linakuja na suluhisho la kulinda kizazi cha nyuki bila kukidhuru kwa moto kama ilivyo kuwa hapo awali lakini pia kulinda mazingira hivyo anawataka walinaji kulichangamkia kununua.

Anaongeza kuwa alilibuni mwaka juzi 2021, wakati chuo hicho chenye idara mbalimbali ikiwamo ya ufugaji wa wanyama na ndege kama kuku, kilikuwa katika mkakati wa kuanzisha ufugaji nyuki pia.

"Nilibuni vazi hili baada ya idara ya mifugo kubainisha mpango wa kuanza kufuga nyuki pia, nikafikiri ni vyema kuwa na vitendea kazi ambavyo vitamkinga mfugaji asing'atwe na nyuki wakati wa kuvuna asali," anasema.

Mbunifu huyo anaendelea kubainisha kuwa anajisikia fahari kwa kuwa ndoto yake ya kubuni vazi hilo imetimia, anafurahi anapoona wafugaji wa nyuki wanaagiza awashonee.

Mwalimu Catherine anasema Chuo cha VETA Singida kinaendelea kulitangaza vazi hilo ili wafugaji nyuki na warina asali wengi zaidi waweze kulifahamu na kulinunua.

Anabahisha kuwa kwa mara ya kwanza alilionyesha wakati wa maonesho ya Sabasaba mwaka 2021, jijini Dar es Salaam, ambapo watu waliotembelea banda la VETA Singida, waliliona na kufurahishwa nalo.

Mwaka huu pia alilipeleka kwenye wiki ya Nyuki Duniani ambayo kitaifa ilifanyika mkoani hapa na kilelele chache kilikuwa Mei 21.



Vazi la kurina asali lililobuniwa na mwalimu Catherine Mtani wa VETA Singida. **PICHA: CLAUDIA KAYOMBO**

"Katika maonyesho ya Siku ya Nyuki duniani tulilipeleka vazi hili kuwapa elimu wafugaji na walina nyuki, kuhusu umuhimu wa kulivaa wakati wa kurina. Baadhi ya wafugaji nyuki binafsi na kutoka maeneo mbalimbali walivutiwa nalo nikawatengenezwa,"anasema.

Anabainisha kuwa mkakati uliopo ni kuendelea kulitangaza ili wahitaji wengi zaidi wafikiwe na taarifa hizo ili waweze kulinunua,

"Tunaendelea kulitangaza, iwapo kutakuwa na maonesho mengine tutaendelea kulitangaza, nina amini wafugaji nyuki wengi wakilijua wataagiza," anasema.

Mwalimu Catherine anaendelea kubainisha kuwa VETA Singida inatarajia kufungua kitengo cha kuzalisha vazi hilo ambapo ili kuwapa fursa wafugaji nyuki katika maeneo mbalimbali kulipata wakati wowote wanaotaka.

Kwa wafugaji nyuki au warinaji walioko sehemu yoyote nchini iwapo wanahitaji vazi hilo anawataka wawasiliane na chuo watashonewa na kukabidhiwa kupitia vyombo mbalimbali vya usafiri wa mikoani ambapo watalipata kwa wakati ila watalipia gharama za usafiri huo.

Akibainisha gharama za vazi hilo mwalimu Catherine anasema kutokana na vifaa vya kushonea vazi hilo kupatikana kwa bei ghali wakati wa maonesho analiuza kwa bei ya Shilingi 80,000, lakini bei halisi ni 120,000.

Akijibu iwapo wanafunzi wake chuoni hapo ameshawaelekeza namna ya kulishona anasema hapana "Wanayojifunza wanafunzi yamo katika silabasi za ushonaji za chuo, hili vazi halipo. Ni ubunifu binafsi" anaongeza mwalimu huyo.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, MAFIA

# Zephania; DC anayebadili matatizo visiwani kuwa fursa za kielimu

WILAYA ya Mafia kisiwa ambacho uvuvi na biashara ya samaki na nazi ni kama kazi ya kila mtu. Na hapo awali shuguli hizo zinaelezwa kuwa zilikuwa kisababishi cha baadhi ya watoto kukatisha masomo.

Mkuu wa Wilaya ya Mafia Zephania Sumaye ambaye ameshika wadhifa huo kwa miezi nane sasa, anaeleza kwamba hali ya utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi na wengine kupata mimba imezidi kudhibtiwa.

Sumaye, anaeleza kwamba vipo vikwazo vilivyochangia kuendelea kuwepo kwa utoro vinavyofanya kazi ili wanafunzi wanaoanza masomo wamalize kwa pamoja kusiwepo na wanaokatisha kwa sababu zinazozuilika

Mipango yake hasa ni kutokomeza utoro na kusimamia kwa karibu suala la elimu kwa kushirikiana na wazazi kuondoa vikwazo vinavyosababisha wanafunzi kukatisha masomo.

Anasema, hali ya utoro kwa shule za msingi ni kidogo kati ya wanafunzi 13,160 na kwamba sababu zinazoelezwa ni pamoja na baadhi ya wazazi kutokuwa na mwamko wa elimu ambao unasababisha kutowafatilia kwenye mahudhurio na maendeleo yao shuleni.

"Kikwazo kingine kinachochangia utoro kinaelezwa kuwa ni ushirikishwaji wa wanafunzi katika shughuli za kiuchumi na kufanyiwa ukatili wa kijinsia pamoja na hali duni ya kiuchumi kwa wazazi na walezi vikisababisha watoto kurubuniwa kwa urahisi na baadaye kukatisha masomo. Malezi mabaya ndani ya baadhi ya familia hasa zisizofuatilia mienendo ya watoto wao wanaporudi kutoka shuleni wapo wanaoonekana kwenye maeneo ya starehe na wengine ujasiriamali" anaeleza Sumaye

Kutembea umbali mrefu kwenye mazingira hatarishi kwenda shule na kurudi nyumbani,kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike ni sababu nyingine anayotaja Mkuu wa Wilaya yote hayo yakichangia kupata ujauzito bila kusahau hali duni ya kiuchumi kwa wazazi na walezi ambayo ni kisababishi cha mtoto kurubuniwa kwa urahisi.



Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Zephania Sumaye.

## KUKABILI UTORO

Anataja kuchukuwa hatua za kisheria kwa watoto, walezi na wazazi kupitia ofisi za kata ili kukomesha tabia hiyo kuwa ni mipango na mikakati ya kukabiliana na visababishi vya utoro Mafia.

"Kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto, wilaya inaendelea kuhamasisha jamii na wadau kuchangia utoaji wa chakula angalau mlo mmoja shuleni ili mtoto aweze kukaa na kujifunza ipasavyo. Kwa kawaida mtoto hajifunzi vizuri akiwa ana njaa, na wakati mwingine kutoelewa masomo darasani kunasababisha watoto kutoroka shuleni, tunaendelea pia na kuhamasisha michezo mbalimbali kwa kutoa vifaa vya michezo ili kuyafanya mazingira rafiki yenye kumvutia mwanafunzi kukaa na kusoma," anaeleza Sumaye.

Anasema halmashauri inaendelea kupambana kupunguza tabia hatarishi zinazosababisha wanafunzi kuacha shule kama vile utoro na mimba za ututoni kwa kuendelea kupunguza umbali wa kutembea kwa wanafunzi kwenda shuleni kwa kujenga shule mpya kwenye maeneo yenye uhitaji mfano shule mpya zinazojengwa katika maeneo ya Sharaza, Skula na Vunjanazi.

Akizungumzia mwamko wa wazazi na walezi kielimu hususan watoto wa kike anasema kwa sasa unaridhisha kwani wanajitoa katika kuwaandikisha watoto wa kike na kwa mwaka huu 2023 na kwamba waliandikishwa asilimia 129.17 kwa elimu ya awali na asilimia101.53 kwa darasa la kwanza, pia wilaya imeanzisha umoja wa wazazi, walezi na walimu katika kukuza ustawi wa wanafunzi shuleni na kupinga ukatili wa kijinsia.

Ofisa Elimu Msingi Wilaya ya Mafia Mohamed Said, anabainisha kwamba kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu ni mwanafunzi mmoja aliyekatisha masomo kwa kupata ujauzito ukilinganisha na mwaka 2022 kipindi kama hicho walipatikana wawili.

Said anaeleza mikakati ya kuinua elimu hususani kwa watoto wa kike kuwa ni kutoa elimu ya malezi na ya uzazi kwa watoto wa kike ili kujikinga na tabia hatarishi zinazoweza kusababisha kuacha shule.

Aidha, hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa kwa watu wanaowafanyia watoto wa kike ukatili wa kijinsia na kuwasababishia kuacha shule, vilevile zitatengwa sh.4,000,000 kuhamasisha jamii kuchangia ununuzi wa taulo za kike shuleni ili kufanya mazingira mazuri ya ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto hao.

Mbali ya mikakati hiyo pia anataja mpango wa kuhakikisha watoto wa kike ufaulu wao unakua ili wawe sawa na wa kiume kwa kuwalea na kuwakinga na tabia hatarishi kupitia walimu wa malezi na ushauri nasaha ili waweze kusoma kama wenzao.

Vilevile kutakuwa na kutoa motisha kwa wasichana wanaofanya vizuri darasani, kazi hiyo ikifanyika shuleni na hata kwenye maadhimisho mbalimbali ya kielimu ikiwemo siku ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Mtoto Duniani ile ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike.

Aidha, anataja kuwapatia mahitaji maalum kama vile taulo za kike chumba maalumu cha hedhi salama shuleni

Akizungumzia suala la uchangiaji wa wazazi kwenye elimu anasema ni wa wastani kwani katika kuwapatia chakula waliochangia asilimia 55 ya wazazi na walezi wote pia katika ujenzi kuna maeneo wanajitoa kikamilifu na nyingine ni kwa asilimia ndogo.

Ofisa Elimu huyo anabainisha vikwazo vilivyopo katika eneo la elimu ya awali na msingi kuwa ni upungufu wa walimu 135 unaosababishwa na kuhamia wilaya nyingine, upungufu wa madawati 924 katika shule za msingi pamoja na vyumba 54 vya madarasa na nyumba 144 za walimu.

Ili kukabiliana na vikwazo hivyo anashauri kuongezewa walimu kukabiliana na upungufu uliopo,kushirikiana kikamilifu na vyombo vya kisheria ili kuharakisha kesi za unyanyasaji wa kijinsia kwa wanafunzi zinafanyiwa kazi na wahusika wanachukuliwa hatua stahiki.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kigambboni Wilaya ya Mafia Hamis Chumu, anasema kuwa awali wanafunzi walikuwa watoro kutokana na majengo kuwa machache na hivyo kulundikana katika darasa moja huku wengine wakikaa chini jambo ambalo kwa sasa limetatuliwa.

Anasema uwepo wa vyumba vingi vya madarasa sambamba na shule kujengwa karibu na wananchi ni jambo ambalo limechangia kuondoa mimba kwa wanafunzi pamoja na utoro kwa wanafunzi wengine.

"Kwasasa wazazi pia wamekuwa na uelewa kuhusu elimu, wakiitwa kwenye vikao wanashiriki na wanachangia michango wanayokubaliana, na hii imesababishwa na uwazi uliopo kwa kuona kila kinachopendekeza kinafanyika wanaona mabadiliko tofauti na zamani" anasema

Rehema Nyalimo, mkazi wa Kilindoni Wilaya ya Mfia anasema tofauti na ilivyokuwa awali sasa hivi wazazi na walezi wamekuwa na mwamko wa elimu na hivyo kushiriki kudhibiti utoro kwa watoto wao.

"Siku hizi watoto wanajitahidi kusoma kwa bidii na hata wakike wanafaulu mpaka daraja A, mimba zimepungua na utoro pia unaenda kuisha kutokana na ushirikiano uliopo kati ya wazazi , walezi na walimu" anasema.

Anawaomba walimu kuendelea kuwa karibu na wanafunzi kwa kuwaelekeza kwa ukaribu ili kuinua kiwango cha ufaulu, kwani katika suala la shule kuwa mbali na makazi limetatuliwa na hakuna kikwazo cha umbali kama ilivyokuwa awali kwa shule za msingi.

ELIMU
NA TUNTU
SWEBE




Mwalimu akifundisha hisabati somo linalodaiwa kuwa adui kwa wanafunzi pengine na watu wengi. **PICHA: MTANDAO**

# Usichukie hisabati unaihitaji ukiwa ndani na nje ya darasa

IMEKUWA ni kawaida wanafunzi kufurahia masomo mbalimbali kama vile English, Kiswahili na Historia, tena wengi wakifaulu kwa viwango vya juu.

Lakini, inapozungumziwa hesabu au hisabati hapo ndipo wengi wanapotamani ardhi ipasuke.

Kwa mfano matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2022 yaliyotangazwa mwanzoni mwa mwaka huu, Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), linaeleza kuwa kati ya wanafunzi 520,556 waliofanya mtihani wa hesabu ambao ni lazima kwa kila mwanafunzi 415, 844 walipata alama F, kwamba walifeli.

Wakati wazazi, walezi, wanafunzi walimu na taifa wanashauri matokeo yatakayotangazwa mwaka ujao, ni vyema kujipa tumaini kuwa mambo yatakuwa mazuri kwa vile juhudi nyingi zinafanyika.

Kwa wanafunzi wengi wanaliogopa somo hilo, kutokana na dhana potofu walizojiwekea au wanazokutana nazo shuleni kuwa hesabu ni ngumu. Wanalipachika somo la hisabati majina kama baba mkwe, ugonjwa wa taifa na gonjwa la moyo.

Yote hayo yanadhihirisha jinsi gani somo hilo lilivyokuwa kero, tishio kama si adui kwa wanafunzi walio wengi kuanzia msingi na hata sekondari.

Fikra hizo husababisha wanafunzi wengi kufeli hesabu kutokana na fikra wanazotengeneza kwenye ngazi za chini hadi juu.

Kwa ujumla wanafunzi walio kote hawazipendi hesabu, hukwepa kufanya mazoezi na yote hayo yakiongeza ugumu kwenye uelewa kwa vile msingi wa kuimudu hisabati ni kujifunza na kufanya mazoezi mara kwa mara.

Wakati mwingine lawama zisiende kwa wanafunzi pia kuna sababu nyingine zikiwamo idadi kubwa ya wanafunzi ndani ya darasa moja na kusababisha kukaa chini.

Huenda hali hii inafanya wanafunzi wasimwelewe mwalimu na nyakati nyingine hasa maeneo yanye joto kali msongamano huo hushusha ari ya kusoma hasa namba au hesabu zinazohitaji utulivu, usikivu na ufuatiliaji.

Katika juhudi na utafiti unaofanyika ili kugundua sababu za kufeli somo la hesabu ni vyema pia serikali na wadau wa elimu kushirikiana kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa madarasa na madawati vitu vinavyoweza kuondoa ari ya kujifunza.

Somo la hesabu linaelezwa kuwa lina upungufu wa walimu. Wapo wachache kuanzia msingi hadi sekondari na kuna wakati inatokea mwalimu mmoja hulazimika kufundisha shule nzima.

Kwa shule za msingi inamaanisha kuwa hufundisha madarasa yote na hata sekondari mikondo yote kwa siku moja jambo ambalo ni gumu na linalochosha.

Ni wazi kuwa jukumu hilo linamchosha na hata kupunguza ufanisi wake wa ufundishaji , baadhi ya wanafunzi kutomwelewa mwalimu na matokeo yake ni kufeli.

Pia, kuna maelezo kuwa huenda walimu hawajui kufundisha licha ya kwamba wenyewe wanaelewa na kuzikokotoa hesabu, lakini wanashindwa kuwafundisha watoto madarasani.

Aidha, hakuna ubishi kuwa hesabu ni ukweli, kama jawabu ni 10 au 200, ukikosea umefeli. Ni ukweli usioweza kubadilika si kama siasa au historia kila mmoja anaweza kuwa na namna yake ya kuelezea na kutoa maoni tofauti na akafaulu pia.,

Changamoto kwenye somo hili la hesabu ni nyingi lakini serikali ifikirie namna bora ya kusaidia kwa kuwapa semina za mara kwa mara kwa walimu ili kukuza maarifa na kuongeza ufahamu.

Pamoja na semina na kozi za kuongeza ufahamu, walimu hao wapate motisha zikiwamo posho na ziara za kujifunza hisabati nje na ndani ya Tanzania.

Ni wakati pia wa kufikiria uwezekano wa kuandaa program maalumu za kuwasaka na kuwafundisha wanafunzi wanaopenda hesabu.

Mbinu hiyo inaweza kufanikishwa kwa kusaka wanafunzi wenye vipaji maalumu kwenye shule za msingi na sekondari na kuwafundisha ili wawe walimu wa ngazi mbalimbali na kuziba pengo la shule zenye uhaba wa walimu wa hisabati.

Mpango huo pia uwahusishe wanafunzi wa kike ambao wanahitaji kupewa hamasa na kuhamasishwa kupenda hisabati kwa kuwa zama hizi masomo hayo ndiyo yenye fursa za ajira, kujiajiri na ujasiriamali unaohusisha ubunifu.

Katika mahojiano na wadau mitaani wanakiri kuwa dunia ya leo hisabati ni muhimu kwa maisha ya kila mmoja, jambo ambalo watu wengi hawajalifahamu. Siyo lazima kuzijua kanuni ngumu mwanafunzi anazozijifunza darasani lakini kujua kuhesabu, kuzidisha na kugawanya ni jambo la kila siku na la kila mtu.

Mwanafunzi Lightiness Mboya, anayesoma shule ya British Mwenge, Dar es Salaam, anasema ukimaliza darasa la saba ukijiunga na Vyuo vya Ufundi (VETA) ukawa mjasiriamali ni lazima kujua mahesabu ili kukadiria mtaji, kufahamu gharama za uendeshaji , mapato na hasara.

Anasema wapo wanafunzi wengi wanaokimbia hesabu lakini ni vyema kuanza kuwa na mtazamo mpya si wa kuiogopa hisabati kwa sababu chochote watakachofanya kinahitaji elimu ya hisabati. Ukiwa fundi ujenzi utalazimika kuhesabu matofali, kukokotoa kiasi cha mchanga, sementi, kokoto na maji.

> Pamoja na semina na kozi za kuongeza ufahamu, walimu hao wapate motisha zikiwamo posho na ziara za kujifunza hisabati nje na ndani ya Tanzania.

Mambo hayataishia hapo kuna hesabu zaidi ili kufanikisha ujenzi wa nyumba kuanzia vipimo, urefu upana na umbo la jengo unalolijenga.

Badhi ya wakulima wa Kyela mkoani Mbeya wanasema kupuuza hesabu kunasababisha wakulima wengi hasa kina mama vijijini kupunjwa, anasema Light.

Mjasiriamali anayeuza tangawizi Manzese, anasema vijana wanaoingia kwenye biashara wanakwama, mtaji kukata kwa sababu hawafahamu hisabati.

Hata ukiuza nyanya, vitunguu, tangawizi lazima ukadirie ufanye hesabu ujue namna ya kupata faida hizo ni hesabu tena huwezi kuzikwepa kwenye biashara zetu, anasema Alice Anyandwile, anayezalisha tangawizi.

"Mfano, una mazao hufahamu biashara, wateja wanapokuja shambani kwako pengine ni wa kutoka nchi jirani ni ujanja. Unaweza kudanganywa kuwa unalipwa kiasi fulani, hujui hesabu . Ukiomba mwenzako unayemwamini akusaidie naye anakupunja kwa vile anafahamu udhaifu wako." Anasema Anakumbusha kuwa kufunga mizigo mikubwa kama rumbesa na kupunja wakulima kunatokana na kutokufahamu hesabu kwa sababu ya kukwepa kutumia mizani.

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Kuzingatia muda wa kulala, kuamka uleule ni tiba, afya



Umaskini unavyochangia watu kukosa pakulala na hata muda maalumu wa kulala usingizi unaohitajika kwa afya. **PICHA: MTANDAO**

KUNA dhana inayotolewa na wanasayansi kwamba ni lazima kulala wakati mmoja kila siku kwa muda wote.

Kadhalika ni afya kuamka muda huohuo wakati wote na siyo kubadilisha badilisha.

Wanasayansi hao wana imani kuwa tofauti ndogo ya mazoea ya kulala kati ya siku za kazi na siku za kupumzika kunaweza kusababisha mabadiliko yasiyofaa ya bakteria au vimelea kwenye matumbo ya binadamu.

Ni kwa mujibu wa utafiti unaofanywa na wanasayansi ukihusisha karibu watu wazima 1,000 uliofanywa na wasomi wa Chuo cha King London, ukibainisha kuwa ratiba za kulała zilizovurugika, hasa kutokana na kazi, zinaleta athari za kiafya kwa wengi bila kuzitaja ni zipi.

Wanashauri kuweka nyakati za kulala na za kuamka zinazofanana ni sawa na kula mlo kamili na kwamba kunaweza kusaidia kupunguza hatari ya kupata magonjwa. Utafiti wao unaeleza kuwa kuna aina mbalimbali za bakteria au vimelea katika mfumo wa usagaji chakula wa binadamu, ambao unaathiriwa na muda wa kulala na kuamka.

> Baadhi ya vimelea hao ni bora au muhimu zaidi kuliko wengine, lakini kupata mchanganyiko sahihi ni muhimu ili kuzuia magonjwa.

Aidha, wanasema baadhi ya vimelea hao ni bora au muhimu zaidi kuliko wengine, lakini kupata mchanganyiko sahihi ni muhimu ili kuzuia magonjwa.

"Mabadiliko ya nyakati za kulała yanaweza kuibua viumbe vidogo vidogo ambavyo vina uhusiano usiofaa na afya yako," anasema Kate Bermingham, mwandishi wa utafiti na mtaalamu wa lishe katika kampuni ya sayansi ya afya ya Zoe.

Anasema, kulala na kuamka nyakati tofauti wakati wa wiki, ikilinganishwa na wikendi, kunadhaniwa kuathiri zaidi ya asilimia 40 ya idadi ya watu wa Uingereza.

Utafiti unafafanua kuwa ni kawaida kwa vijana kulala na kuamka muda tofauti na kisha hali hiyo hupungua kadri wanavyozeeka. Washiriki wa utafiti huo uliochapishwa na Jarida la European Journal of Nutrition, walichunguza usingizi na damu.

Wanasema sampuli za kinyesi zilikusanywa na kurekodi kila kitu walichokula katika dodoso la chakula. Wale ambao hubadilisha nyakati za kulala kwa asilimia 16 wana uwezekano wa kula chakula kilichojaa viazi, ikiwa ni pamoja na chips, pamoja na vinywaji vya sukari, matunda pamoja na karanga.

Wanasema utafiti wa awali ulionyesha kuwa watu wanaobadilisha nyakati za kulała hula vyakula kidogo vya nyuzinyuzi kuliko wale ambao nyakati zao za kulała hazibadiliki.

Aidha, wanasema utafiti mwigine uligundua kuwa watu wanaobadili muda wa kulala hupata uzito zaidi, magonjwa na uchovu wa akili.

Halikadhalika watatafiti waligundua jamii au spishi tatu kati ya sita za viumbe vidogo vidogo au vimelea zilikuwa nyingi zaidi kwenye matumbo ya watu wanaobadili nyakati za kulała. Vilevile wanahusishwa na lishe duni, kunenepa, viwango vya juu vya maambukizi na hatari ya kupata kiharusi.

"Kudumisha utamaduni wa kulała wakati huo huo na kuamka muda huo huo katika maisha, ni tabia inayoweza kufuatwa kwa urahisi," anasema Dk Sarah Berry, wa Chuo Kikuu cha King London.

Watafiti hao wanasisitiza kuwa kudumisha nyakati za kulala na kuamka bila kubadilika na kupata usingizi wa kutosha ni ufunguo wa kuwa na afya bora ya akili na kuhisi kuwa umeburudishwa na kutiwa nguvu kila wakati.

Wanakumbusha kuwa kufuata muda wa kawaida wa kuamka asubuhi ni mojawapo ya mambo bora zaidi unayoweza kufanya ili kuboresha usingizi wako usiku wa siku inayofuata.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linaeleza kuwa kiwango cha chini kinachopendekezwa kwa kila usiku kwa watu wazima kulala ni saa saba.

Aidha, watoto wanaokwenda shule wanapaswa kulala kati ya saa 2:00 na 3:00 , wakati vijana wanashauriwa kwenda kitandani kati ya saa 3:00 na 4:00 usiku wakati watu wazima wanapaswa kulala kati ya 4:00 na 5:00 usiku.

Suala la mlo wa usiku nalo linatajwa ikielezwa kuwa ni vyema kuzingatia lishe yenye afya kwa mfano kula angalau aina tano za matunda na mboga kila siku

Aidha, weka matunda na mboga nyingi zaidi kwenye vyakula vyenye wanga mwingi kama vile viazi, mkate, chapati, ugali wali au tambi.

Lakini pia inashauriwa kula vyakula mbadala vya maziwa au kunywa maziwa na kula mlo wenye sukari au mafuta kidogo kila mara inapowezekana.

Kadhalika, ni vyema pia kuzingatia kula maharage, kunde na jamii zote za mikunde, pia samaki, mayai, nyama na protini nyingine bila kasahau kunywa maji mengi walau glasi sita hadi nane kwa siku. **BBC**

## Ubunifu kuvuna asali ulivyonusuru nyuki, wafugaji na kuokoa misitu

**INATOKA UK.11**

Akijibu iwapo wanafunzi wake chuoni hapo amesha waelekeza namna ya kulishona anasema hapana "Wanayojifunza wanafunzi yamo katika silabasi za ushonaji za chuo, hili vazi halipo. Ni ubunifu binafsi" anaongeza mwalimu huyo.

Anatoa wito kwa wanaolihitaji wengine ambao hawakuwa wanafahamu iwapo chuo hicho kimekuja na suluhisho la namna bora ya kurina asali kirafiki, kuagiza vazi hilo kwani yupo tayari kulitengeneza.

Michael Lyagula, ni mwalimu wa Idara ya Ushonaji anayesema kubuniwa kwa vazi hilo ni hatua kubwa katika kazi yao na kwamba pamoja na mambo mengine mkoa wa Singida ni miongoni mwa mikoa nchini inayofuga nyuki kwa wingi hivyo ana amini miongoni mwa wateja wa watatoka kwa wingi mkoani humo.

Akizungumzia bei Lyagula anasema inapangwa kutokana na gharama ya malighafi inayotumika kulitengenezea vazi hilo ambalo rafiki wa kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Anawataka wafugaji nyuki na warina asali kulitumia ili kuwarahisishia kazi mbapo sasa hawatatumia muda mrefu kwa ajili ya kufanya maandalizi kabla ya kupata asali kwenye mizinga iwe ni kupakua asali yote, kuchukua kiasi na kukagua mizinga mashambani.

Kutoka kwa Kaimu Mkuu wa Chuo, Alphoncina James, anawapongeza walimu kwa ubunifu hasa Catherine kwa hatua ya kubuni vazi hilo huku akihamasisha wanafunzi na walimu kuendeleza bunifu mbalimbali.

"Kama chuo tunahamasisha walimu na vijana wetu wagundue teknolojia mbalimbali, mambo ambayo yataongeza ufanisi na tija kwa chuo na Watanzania" anasema Alphoncina.





## W'biashara wadaiwa kuchanganya mbaazi, kunde gunia moja

**Na Augusta Njoji,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma, Remidius Mwema, amebaini kuwapo na mtandao wa wafanyabiashara wanaoharibu taswira ya Soko la Kimataifa la Mazao la Kibaigwa kwa kuchanganya mbaazi na kunde kwenye gunia moja.

Akizungumza jana na wafanyabiashara wa soko hilo, Mwema alisema kutokana na kuibuka kwa vitendo hivyo, Polisi wilayani hapa wamefanya msako na kuwakamata wafanyabiashara wakiwa na magunia ya mbaazi yaliyochanganywa na kunde.

Alisema kitendo hicho ni kuhujumu soko na anafahamu kuna kambi zipo maeneo ya soko na kufanya kazi ya kuchanganya mazao hayo.

"Mwenye kulitenda hili na wenye mazao haya wanaofanya hivi waache mara moja, hatachelewa kuwachukulia hatua watu hawa,"alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara sokoni hapo, James Ikanda, alisema kuna wafanyabishara ambao siyo waaminifu wamekuwa pia wakichanganya na mchanga hali ambayo inalitia doa soko hilo.

Mkazi wa Kibaigwa, Sipendeki Ramadhani, alisema kuna uwezekano mkubwa wa kuwapoteza wafanyabishara na kulichafua soko kimataifa.

# Watu wenye ulemavu walia kutoshirikishwa katika mipango

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU wenye ulemavu mkoani Singida, wamezitupia lawama serikali za mitaa wakisema haziwashirikishi kwenye mipango ya maendeleo kutokana na kasumba iliyojengwa kwamba ni wasumbufu, hali inayowafanya wakose haki za kiuchumi.

Walieleza hayo mwishoni mwa wiki kwenye uzinduzi wa mradi wa uongozi na haki za kiuchumi kwa wanawake utakaotekelezwa mkoani hapa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojishughulisha na masuala ya wanawake (UN WOMEN) na Shirika la Maendeleo ya Jamii la TUSONGE kwa ufadhili wa Serikali ya Finland.

"Viongozi wa serikali za mitaa kimsingi wamekuwa hawawashirikishi watu wenye ulemavu kwenye mipango ya maendeleo wanawatenga," alisema Ziada Nsembo ambaye ni mlemavu wa ngozi.

Naye, Rehema Hassan alisema serikali za mitaa haziwashirikishi katika mipango ya maendeleo kutokana na kuwachukulia kama ni watu wabishi ambao wamekuwa wakihoji mambo mengi kwenye vikao na mikutano.

Alitoa ushuhuda wa jinsi unyanyasaji unaofanywa kwa wanafunzi wenye ulemavu, akisema katika shule moja iliyopo Manispaa ya Singida mwalimu alimtoa kukaa mbele darasani na kumpeleka nyuma mwanafunzi mwenye ulemavu ambaye baadaye alimua kuhamia katika shule moja iliyopo wilayani Ikungi.

Husna Abdallah alisema wakati anasoma katika shule moja Mkuu wa Shule ya Sekondari iliyopo wilayani Mkalama aliwadharau wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi kwa kuwaambia kuwa wamelaaniwa hali iliyosababisha wanafunzi 11 wenye ulemavu kususa chakula cha shule.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la TUSONGE, Agnatha Rutazaa, alisema wanawake wakijumuishwa kwenye maamuzi kuanzia ngazi za chini itasaidia kuleta sera zenye kuheshimu usawa wa kijinsia katika jamii ya kitanzania.

Alisema: "Serikali za mitaa ndio chimbuko la mifumo dume kandamizi ambayo inatokana na mila na desturi kwa hiyo shirika la TUSONGE litafanya kila jitihada kupambana na changamoto hiyo ili kuwe na usawa na idadi kubwa ya wanawake waweze kushiriki kwenye uongozi".



Baadhi ya watumishi wa umma wakishiriki semina iliyoandaliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) kwa ajili ya wastaafu watarajiwa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TPHPA wafanya ukaguzi maduka 1,056 ya viuatilifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), imefanya ukaguzi wa maduka 1,056 yanayouza viuatilifu kwenye wilaya 72.

Lengo la ukaguzi huo ni kuhakikisha wanauza viuatilifu vyenye ubora kwa wakulima kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo.

Kaimu Mkurugenzi wa TPHPA, Prof. Joseph Ndunguru, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kuhusu mikakati mbalimbali waliojiwekea kwa ajili ya kukabiliana na wadau waharibifu wa mimea katika mazao mbalimbali nchini.

Alisema lengo la kufanya ukaguzi huo ni pamoja na kutaka wauzaji wa bidhaa hizo wawe wamesajiliwa ikiwemo kuwa na vibali, lakini pia wauze bidhaa bora ambazo zitamfanya mkulima aendeshe kilimo chenye tija ambacho kitamuinua kiuchumi.

"Tumefanya ukaguzi katika mikoa hiyo, bado tunaendelea na mikoa mingine ili kuhakikisha wafanyaiashara wa viuatilifu wanauza bidhaa bora kwa wakulima," alisema Prof. Ndunguru.

Alisisitiza kuwa moja ya kazi kubwa ya mamlaka hiyo ni kuhakikisha viuatilifu ambavyo vinasambazwa kwa wakulima vinakuwa na ubora unaotakiwa na wanafanya ili kuhakikisha wakulima wanapiga hatua kwenye kilimo biashara.

Aidha, alisema tayari mamlaka hiyo imetoa elimu ya kunyunyizia

dawa ya kukabiliana na wadudu waharibifu kwenye zao la korosho kwa wakulima 841 katika mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara.

Alifafanua kuwa TPHPA inafanya hivyo ili kuhakikisha wakulima

wanaposafirisha mazao yao nje ya nchi kwa ajili ya kuuza yanakuwa hayana kasoro yote katika soko la ushindani wa mazao.

"THPHA inafanya hivyo ili kuhakikisha wakulima hawakwami katika soko la mazao yanaokwenda nje na uwezo huo tunao kwa sababu serikali imetuwezesha vifaa vya kisasa vya kufanya kazi hiyo," alisema Prof. Ndunguru.

Alisema korosho ni zao la biashara na la kimkakati, hivyo

wakulima wake wanapaswa kuwa mstari wa mbele kutumia viuatilifu kwa ajili ya kukabiliana na wadudu waharibifu wa mazao.

Kadhalika, alisema wamekuwa wakifanya udhibiti wa wadudu waharibifu kama nzige na kwelea kwelea kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali hapa nchini, ambao zinatoa taarifa kama kuna eneo lina viashiria vya wadudu hao waharibifu wa mazao ya mimea.

Alisema wadudu hao wanadhibitiwa kupitia ndege zisizo na rubani ambazo wamekabidhiwa na serikali kwa ajili ya kukakabiliana na wadudu hao waharibifu wa mazao.

Profesa Ndunguru: "Tunaishukuru sana serikali kwa kuiwezesha mamlaka vifaa vya kisasa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa wakulima na wafanyabiashara wanaoutegemea".

## Serukamba awashukia wahandisi wanaokwamisha miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewashukia baadhi ya wahandisi katika halmashauri za wilaya kwa kuwa chanzo cha kuchelewesha kukamilika miradi.

Serukamba alitoa kauli hiyo juzi alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa ujenzi wa nyumba za walimu na sekondari mpya katika Halmashauri za Wilaya ya Ikungi, Manyoni na Itigi.

Miradi hiyo inajengwa kwa fedha zilizotolewa na serikali kupitia Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Alisema kuwa wahandisi wa halmashauri wanatakia kuwakagua mafundi, kuwasimamia kuwashauri, kuwapangia majukumu na kuona hatua za utendaji kazi zinavyoendelea pamoja na kiwango cha utendaji ili kuharakisha ujenzi wa miundombinu hiyo ya shule kutekelezeka kwa ufanisi.

"Miradi mingine inachelewa kukamilika kwa wakati katika baadhi ya halmashauri kwasababu wahandisi ambao wana wajibu wa kusimamia mafundi hawaendi kwenye miradi kukagua kuona maendeleo badala yake wanakaa tu ofisini,hili halikubaliki lazima wahandisi mbadilike," alisema.

Aliwagiza wahandishi ifikapo Septemba 30, mwaka huu miradi yote ya SEQUIP iwe imekamilika na baada ya hapo hatataka kusikia visingizo vyovyote.

Serukamba alisema wahandisi wahakikishe kila siku wanakwenda kutembelea miradi hiyo na kukusanya taarifa kila jioni ili kuona ni mkandarasi au fundi gani ambaye anakwamisha miradi hiyo na ikibidi anyang'anywe mradi na kupewa mtu mwingine ambaye anaonesha nia ya kumaliza kazi mapema.

Serukamba alisema mkandarasi ambaye anafanya kazi kwa kusuasua na kufanya kazi chini ya kiwango hatavumiliwa kwani ni lazima thamani ya fedha ionekane na miradi iishe kwa wakati ili walengwa waweze kutumia madarasa hayo.



# TRA yazindua kampeni maalum uhamasishaji utii sheria za kodi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Mbeya, imezindua kampeni maalumu ya kuhamasisha wafanyabiashara kutii sheria za kodi, ikiwemo kutoa risiti kila wanapouza bidhaa zao ili kuepuka kukumbwa na mkono wa sheria.

Aidha, elimu hiyo inatolewa pia kwa wananchi kudai risiti wanaponunua bidhaa madukani ili kuisaidia serikali kukusanya mapato pamoja na kuepuka kununua bidhaa zisizokidhi viwango.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo ijulikanayo kwa jina la 'Tuwajibike' Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Msibu Shaaban, alisema kampeni hiyo inalenga kuwahamasisha walipakodi kutii sheria bila shurti.

Alisema kwa sasa wanatoa elimu kwanza ili wananchi waelewe kabla ya kuanza kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo za kisheria jambo ambalo alisema siyo kipaumbele.

Hivyo, aliwataka wafanyabiashara kuhakikisha wanasajili biashara zao, wanakuwa na namba ya mlipakodi pamoja na kulipa mapato wanayokuwa wamekadiriwa kwa wakati.

Alisema kampeni hiyo inalenga kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi kutoa elimu hiyo hasa kuhusu kutoa na kudai risiti za kielektroniki (EFD).

"Maofisa wetu wa TRA watatembelea maeneo mbalimbali kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi ili kuhakikisha wote tunakuwa na uelewa wa pamoja, tunataka wananchi waelewe kwamba risiti ndiyo maendeleo yao," alisema Shaaban.

Alisema moja ya madhara ya mfanyabiashara kuuza bidhaa bila kutoa risiti ni pamoja na kutozwa faini ambayo alisema wakati mwingine huwa haiendani na kiwango cha fedha za bidhaa wanazokuwa wameuza.

Alisema wananchi wote wakiwa na uelewa itasaidia kupunguza hata biashara za magendo ambazo zimekuwa zikifanyika hasa maeneo ya mpakani.

Naye Meneja Msaidizi wa TRA kitengo cha Ukaguzi, Mygloria Saria, alisema mfanyabiashara anapobainika kuuza bidhaa bila kutoa risiti adhabu yake ni faini ambayo ni asilimia 20 ya thamani ya bidhaa iliyouzwa.

Vilevile alisema mnunuzi ambaye anabainika kununua bidhaa bila kudai risiti adhabu yake ni asilimia 20 ya thamani ya kodi iliyopotea kwa kutodai risiti ama Sh. 30,000 faini ambazo alisema wakati mwingine haiendani na bidhaa.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanafuata sheria hizo ili kuepuka kukumbwa na adhabu hizo ambazo alisema wakati mwingine zinaweza kudidimiza bidhaa zao.

"Kwahiyo sasa hivi tumeamua kuwekeza kwanza kwenye elimu ili wananchi waelewe, adhabu zinazotolewa tunataka iwe ni jambo la mwisho kabisa," alisema Mygloria.

Akizindua kampeni hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliwataka maofisa wa TRA kupita katika maeneo yote ya biashara na kuwasaidia wafanyabiashara kutatua kero zote ambazo zimekuwa zikikabili biashara zao.

Vilevile aliwataka kusisitiza umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati akidai kuwa maendeleo ya nchi yanategemea kodi ambazo zinatolewa na wananchi kupitia kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Aliwataka wananchi kutowaogopa maofisa wa TRA wanapoingia kwenye maeneo yao kwa maelezo kuwa wanapita kwa lengo la kutoa elimu.

Alisema kodi wanayolipa ni kwa ajili ya maendeleo ya taifa na hivyo akawataka kutoa taarifa zao sahihi zinazowezesha biashara zao kukua.

"Ukitoa risiti na kudai risiti unakuwa ni mzalendo wa kweli kwa taifa letu lakini ukifanya kinyume unakuwa umeshiriki kuhujumu taifa," alisema Homera.

Baadhi ya wafanyabiashara walisema elimu hiyo inayotolewa na maofisa wa TRA itawasaidia kupata uelewa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu kodi na madhara ya kutotoa kodi.




Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi ya Paradise Mission iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, akielezea kuhusu moyo na kazi zake mwishoni mwa wiki katika mahafali ya pili ya darasa la saba shuleni hapo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wazazi, walezi wapewa angalizo malezi ya watoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZAZI na walezi wametakiwa kuwalea watoto wao kwa umakini, kuwa karibu nao ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili ikiwemo ubakaji na unajisi.

Ofisa Taaluma Msingi wa Jiji la Mbeya, Neema Njavike, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya pili ya darasa la saba ya Shule ya Awali na Msingi ya Paradise Mission iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya.

Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwatelekeza watoto wao bila kuwafuatilia michezo na wanaoshinda nao hali ambayo alisema inachochea vitendo viovu dhidi yao.

"Niwasihi sana wazazi na walezi kuweni karibu na watoto wenu kwa sababu watoto wanatendewa vitendo vibaya sana, hii ni kutokana na kwamba mnakaa mbali na watoto wenu bila kuwafuatilia na kuwadadisi," alisema Neema.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Rosarina Mtumbuka, alisema malengo ya shule ni kuhakikisha wanafuzi wanapata elimu na malezi bora ambayo yatawafanya kutimiza ndoto zao za maisha.

Alisema shule imejikita kwenye michezo ambayo inawafanya wachangamshe akili zao na kuwa na afya njema wawapo shuleni pamoja na kuhakikisha kila mtoto anafuatiliwa na kutatuliwa matatizo yake.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya, Akimu Mwalupindi, aliwataka viongozi wa Serikali ya Kata ya Nsalala kushirikiana na Shule ya Paradise Mission kwa kuhakikisha watoto wote wanakuwa salama.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Ndele Mwaselela, alisema amekuwa akiyatumia mapato yatokanayo na shule hiyo pamoja na shule ya Patrick Mission iliyopo jijini Dar es salaam kusaidia watoto wasiojiweza.

Alisema mpaka sasa amesomesha zaidi ya watoto 500 ambao wamefikia ngazi mbalimbali za elimu na kwamba hata maendeleo mengine kwenye jamii amekuwa akichangia.

# RC akemea tabia wanawake kutonyonyesha watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, amekemea tabia ya baadhi ya wanawake kukwepa jukumu la kuwanyonyesha watoto wao kwa kisingizio cha kufanya kazi za kujitafutia kipato.

Mtaka alikemea vitendo hivyo mwishoni mwa wiki wakati wa kufunga makambi ya Kanisa la Waadvetista Wasabato, aliwataka kinamama kutenga muda kwa ajili ya kuwalea watoto wao.

"Mkoa wa Njombe wanaoongoza kwa kumiliki uchumi ni kina mama na akishajifungua anapika makande anaacha ndani wiki nzima mtoto anakula makande kuanzia asubuhi mpaka asubuhi, wiki nzima yeye yupo kwenye kutafuta,matokeo yake watoto wanapata shida ya afya,"alisema Mtaka.

"Sasa niwaombe Doricas, Mwenyekiti, viongozi naomba tupate muda tuwainjilishe kinamama wa Mkoa wa Njombe kwenye zile siku 1,000, maana ya ujauzito, namna ya kumuandaa mtoto akiwa tumboni na namna ya kulea mtoto baada ya kujifungua miaka ile mitano ya kwanza"alisema Mtaka.

Alisema ni vema jamii ikasaidiana namna ya kuwalea watoto pamoja na namna ya kinamama kuandaa chakula baada ya kujifungua na kwa watoto wanaowanyonyesha.

"Na suala zima la unyonyeshaji kwa watoto lakini mchungaji umezugumza pale kwamba kanisa linakemea mambo ya ovyo, mambo yasiyokua ya kimaadili kama ushoga na usagaji. Viongozi jambo hili limezungumzwa kitaifa siyo kwamba sisi Njombe ni kisiwa kwa hiyo ni lazima tuwe na wajibu pia wa kusaidia jamii yetu nje ya kanisa kwenye suala la maadili na malezi ya watoto" alisema Mtaka.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika aliwataka wazazi kushirikiana katika malezi ya watoto ili kukabiliana na tatizo la udumavu.

"Bado tunatatizo la udumavu katika familia zetu, wazazi wetu na hasa kinamama maana yake matunzo ya mtoto ni ya baba na mama lakini mama ndio hasa kiini cha matunzo, hivyo wahakikishe wanawapa watoto lishe kwa wakati ili kuondoa tatizo la udumavu" alisema Mwanyika.

Mchungaji Richard Mashauri, alisema wiki nzima mwamko umekuwa ni mkubwa katika kueneza neno la Mungu pamoja na kuwaasa wananchi kuepukana na matukio ya kihalifu na mauaji.

Alisema "Nawasihi Watanzania katika kuhitimisha makambi haya kila jambo tuanze na Mungu, kwa kila maamuzi, kwa kila tendo mnalotenda, watu wa Njombe waendelee kwa baraka ambayo Mungu ametupatia ya kuzaa lakini tuwatunze hawa watoto".

# Wizara ya Ujenzi yaendelea kujenga uchumi wa kidijitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema inaendelea kujenga uchumi wa kidijitali katika kuleta maendeleo kwa kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za serikali na wananchi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa wizara hiyo, Dk. Khalid Salum Muhammed, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Wawi, Bakari Hamad aliyetaka kujua mikakati ya serikali ya kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza kupitia matumizi mabaya ya teknolojia mpya ya kidigitali.

Dk. khalid alisema, Serikali kupitia Shirika la Mawasiliano (ZICTIA) imeweka sera na sheria ili kudhibiti athari mbaya zinazoweza kutokea kutokana na matumizi mabaya ya teknolojia mpya za kidijitali.

Aidha, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia ZICTIA inaendelea kuwajengea uwezo watendaji wa Shirika la Mawasiliano (ZICTIA) pamoja na kuweka mifumo bora itakayoweza kudhibiti athari mbaya ya matumizi ya teknolojia mpya ya kidijitali.

Pia alisema Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 inatoa fursa ya ulinzi wa taarifa kwa wananchi wa kawaida ambaye ataona kwamba haki zake au taarifa zake, zimepotoshwa, ama kuna kampuni ilichukua taarifa kwa lengo fulani na badala yake kuzitumia kwa lengo lingine.

# Polisi yataja chanzo kushamiri kwa matukio ya uhalifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limesema kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu visiwani humo kunatokana na wananchi kutohudhuria mahakamani kutoa ushahidi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Richard Thadei Mchomvu, aliyasema hayo wakati alipofanya kikao na wananchi wa Kinuni, Pangawe, Mnarani na Mwembe Majogoo katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Kamanda Mchovu alisema Jeshi la Polisi linaendelea na mikakati ya kuzuia na kupambana na uhalifu na udhalilishaji ndani ya mkoa huo kwa kuwashirikisha wananchi katika ulinzi shirikishi ili kubaini na kutatua changamoto za uhalifu.

Alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo katika kuondoa vitendo vya uhalifu ni kukosa ushirikiano wa wananchi wanapohitajika mahakamani kwa ajili ya kutoa ushahidi, hivyo hupelekea watuhumiwa kushindwa kutiwa hatiani.

"Kuna matukio kadhaa ya kihalifu yalitokea katika maeneo yenu, wananchi waliyaona na kuwakamata watuhumiwa na kuwafikisha vituo vya polisi, hilo mnalifanya vizuri sana katika kupambana na uhalifu. Changamoto iliyopo ni kwamba mkifikisha watuhumiwa kituoni mnakuwa wagumu kwenda mahakamani kutoa ushahidi hivyo kupelekea kesi hizo kufutwa na wahalifu kurudi mitaani kuendelea na uhalifu" alisema Kamanda Mchomvu.

Aidha, Kamanda huyo alisikitishwa na vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wananchi kufuta kesi kwa kuogopa muhali katika jamii hali ambayo inawapa mwaya wahalifu kuendelea na vitendo hivyo.

"Hapa nina majalada ya kesi zilizofutwa ambazo wananchi wa maeneo haya ya Kinuni na Nyarugusu wamefuta kesi kwa kuogopa muhali. Kuna kijana hapa alishambuliwa na wahalifu saba lakini mama mzazi wa kijana huyo akaamua kwenda Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwenda kufuta kesi ili wahalifu hao wote waendelee tu kufanya uhalifu," alisema Kamanda Mchomvu.

Aidha alisema baadhi ya wananchi wanaungana na kwenda kumuomba mlalamikaji ili kufuta kesi na asipofanya hivyo wanamtenga katika jamii jambo ambalo linaleta hofu kwa mlalamikaji, hivyo kuamua kufuta kesi hizo na mhalifu kuendelea kufanya uhalifu.

"Wahalifu waliopo katika maeneo yetu ni zao la jamii yetu sisi wenyewe, hivyo kuendelea kuwalea na kuoneana muhali haiwezi kuwa kinga ya kumaliza uhalifu katika maeneo yetu, jamii lazima iamke na kuchukua hatua za kisheria ili kukomesha vitendo hivyo," alisema.

Akijibu swali la mwananchi aliyeeleza kwamba baadhi ya askari kutotoa huduma nzuri vituoni, Kamanda Mchomvu alisema katika vituo vyote vya Polisi vina namba za simu za viongozi, hivyo aliwataka wananchi kupiga simu kwa namba hizo pindi wanapokutana na huduma isiyoridhisha katika vituo hivyo ili hatua stahiki zichukuliwe kwa haraka.

"Nawaomba wananchi mnipigie simu muda wowote mnapokutana na huduma isiyoridhisha kwenye vituo vya Polisi, pigeni ile namba iliyoandikwa RPC inapatikana saa 24 hata iwe saa nane usiku nipigie nitakusaidieni," alisema.

Akitolea ufafanuzi kuhusu changamoto ya uwepo wa usafiri katika vituo vya Polisi ambapo wananchi wamelalamika kuwa wanapowakata watuhumiwa kuna uchelewaji wa usafiri, Kamanda Mchomvu alisema Jeshi la Polisi kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi limeagiza magari na pikipiki za kutosha ambazo zitakuja kumaliza tatizo hilo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Magharibi B" Unguja, Hamida Mussa Khamis, amelipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya vikao vya kusikiliza changamoto za kiusalama katika maeneo ya mkoa huo pamoja na kutoa elimu ya Polisi Jamii ambapo amesema kwa kiasi kikubwa inaleta matokeo chanya.

Alisema changamoto ya vikundi vya ulinzi shirikishi kutokuwa na ofisi, Serikali imeahidi kujenga ofisi za masheha ambapo katika mpango wa awamu ya kwanza zitajengwa ofisi 75, ambapo Wilaya ya Magharibi B" imepata nafasi ya kujengewa ofisi za Masheha na amefafanua kwamba ofisi hizo zitatumika pia na vikundi vya ulinzi shirikishi katika kutimiza majukumu yake.

Mkuu wa Polisi Jamii Mkoa wa Mjini Magharibi, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Cleophance Magesa, alisema wazazi na walezi wanapaswa kuimarisha malezi bora ili kuwajenga watoto katika maadili mema.




Mbunge wa Malindi Zanzibar, Mohamed Suleiman Omar (wa pili kushoto), akikabidhi moja ya vifaa vya muziki kwa kiongozi wa Kikundi cha Taarabu cha Nadi Ikwan Safaa, Mariamu Hamdani, alipowatembelea Kokoni mjini Zanzibar jana. Kushoto ni mwimbaji wa taarabu Mohamed Ilyasi na kulia ni Katibu wa kikundi hicho, Ahmed Juma Mohamed. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Gharama kubwa yatajwa kikwazo vyeti vya kuzaliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) imesema bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi, kwa sababu jamii haina elimu ya umuhimu wa vyeti hivyo pamoja na kushindwa kumudu gharama zake.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waratibu wa wanawake na watoto wa mikoa mitatu ya Unguja katika mkutano wa kujadili kazi zinazofanywa na jumuiya hiyo kupitia mradi wa kuwawezesha wanawake katika masuala ya uongozi (SWILL).

Alisema changamoto ya jamii kutokuwa na vyeti vya kuzaliwa ipo zaidi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, hivyo ni vyema hujudi zikafanyika katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa vyeti hivyo.

"Wengi wao wamekua wakijitokeza kufuatia upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa hadi pale watoto wao wanapofika darasa la saba na kulazimika kupeleka vyeti vya kuzaliwa shuleni ili kufanya mitihani hao ya taifa," alisema Jamila.

Aidha, alisema wakati umefika kwa wadau mbalimbali wa haki za wanawake na watoto kushirikiana na serikali katikak kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa ili kila mwananchi kuwa na cheti hicho.

"Lazima vyeti tuvitunze vizuri kwa sababu wapo ambao walikuwa navyo vyeti hivi lakini sasa hawana kutokana na sababu mbalimbali aina kwa kupotea, kuchakaa na kuliwa na panya majumbani kutokana na kutoa na udhibiti mzuri," alisema Jamila.

Jamila alisema ili jamii ihamasike kuwa na vyeti vya kuzaliwa lazima kuondosha vikwazo vivilivyopo ikiwemo kuchelewa upatikanaji wake hali ambayo huwavunja moyo wananchi kufuatilia.

Mratibu wa Wanawake na Watoto Shehia ya Kikungwi Mkoa wa Kusini Unguja, Bahati Issa, aliiomba serikali kupunguza gharama za upatikanaji wa vyeti hivyo kwa sababu baadhi ya jamii hawana uwezo wa kumudu gharama ya Sh. 42,000 kwa ajili ya kupata vyeti.

"Unamkuta mzazi mmoja anawatoto watano na wote hawana vyeti vya kuzaliwa, hivyo gharama hii ya Sh. 42,000 kwa kila cheti kitamshinda kumudu gharama hizi," alisema Bahati.

Akiwa katika mikutano yake ya kusikiliza kero za wananchi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mkuu wa Mkoa huyo, Ayoub Muhammed Mahmoud alikiri uwepo wa tatizo la wananchi wengi wa mkoa huo kutokuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Alisema miongoni mwa sababu ni kuchelewa kwa upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kunakotokana na waombaji kushindwa kulipia gharama za kupata cheti.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**GLADYS KIBIRA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0534-0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. **ANTHONY'S SEC SCHOOL - MBAGALA** mwaka 2003. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MTW/MTW/527/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPHINE G MACHABA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index S1474-0015 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari **WHITE LAKE** mwaka 2009,yeyote atakaye kiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **PHQ/DAR/KIN/16513/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EMANWELY PATRICK MWAMLIMA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 478 CVT** aina ya **BOXER 125X.** yenye CHASSIS NO. **86608.** ENGINE NO. **JVXWLH14325.** Yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/DAR/UBU/16900/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CHARLES MIHANA MOSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC. 655 BTL** aina ya SUNLG, yenye Chassis No. **LTZPCKLN0H6200392**, Engine No. **162FMJH0000572,** Model **No. SL150-5.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kiichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **KAS/RB/2610/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MBAZI STEVEN MRITA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 149 DFT** aina ya **TOYOTA CARINA** yenye Chassis No. **AT210056397.** Engine No. **5AH261366.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/3027/2023**

---

**MAHAKAMA YA WILAYA YA SINGIDA**
**MKOA WA SINGIDA**

**HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI Na 28/2023**

**OMBI LA BASILISA MWAMBURA DAFFI KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU JASTINI JUMANNE SAMWAJA.**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote wa mirathi ya marehemu JASTINI JUMANNE SAMWAJA wanaalikwa kuja mahakamani kuhudhuria kesi mnamo tarehe 02 mwezi 10 mwaka 2023, Kabla mwombaji huyo hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

Tarehe 14/09/2023

............................
Hakimu mkazi
Mahakama ya Wilaya Singida

THE DISTRICT COURT OF SINGIDA TANZANIA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA WILAYA SINGIDA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 94 of 2023**

**In the Matter of the Estate of the LATE MERYSIANA GIDEON CHIKOTI Of Chamwino within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by FANUEL KEPHA BWANA MZURI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 04 day of 10......................... 2023

**Dated at Dodoma this 13 day of 09................2023**

COURT SEAL DODOMA DISTRICT
RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MUHEZA**

**Kituo cha NGOMENI Mkoa TANGA**

**Shauri la Madai Na. 19/2023**

**Jina la Mdai: MOHAMED OMARY MBWANA**

**Jina la Mdaiwa: (1) OMARY MIRAMBO (2) MAUA SAID**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: OMARY MIRAMBO**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai Ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba MADAI YA TSH. 3,000,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 Mwezi wa 9 Mwaka 2023 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 21 Mwezi 9 Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NGOMENI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA**
**Mkoa TANGA**

**Usimamizi wa mirathi Na.....170.../2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RASHIDI ABDALLAH SAMPA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA OMARI MHINA KISAVULE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 2 mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 25 Mwezi 9 Mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO TANGA MJINI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA WITO MBELE YA TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI.**
**(IMETENGEZWA CHINI YA KANUNI YA 34(1))**

**MGOGORO WA KIKAZI NA. CMA/MZA/NYAM/12/2014**

**MHUBIRI ROGEGA MONG'ATEKO...MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MAK MEDICS LTD....MJIBU MAOMBI**
**(TAARIFA YA KUITWA KUHUDHURIA KWENYE SHAURI LA USULUHISHI)**

UNAARIFIWA KUWA SHAURI LILITOJWA HAPO JUU, LINALOKUJA KWA KWA HATUA YA USULUHISHI /UAMUZI, LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 29/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI MAHALI NI OFISI ZA CMA-MWANZA.

IMETOLEWA NA KUGONGWA MUHURI LEO TAREHE 25/09/2023.

JINA: MHESHIMIWA WANDIBA SAHIHI:

AFISA MASIJALA/MSULUHISHI/MUAMUZI

FOMU YA KUPOKELEWA KWA HATI YA WITO(ITAJAZWA NA MPELEKAJI WA HATI HIYO)

JINA: MARWA CHACHA KISYERI CHEO : P/REPRESENTATIVE

SAHIHI: TAREHE:25/09/2023

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 89 LA MWAKA 2023**

**JUMA SAID KADINGO...........MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**(1) FARAJ ALLY SAEED**
**(2) REHEMA MWINYIJUMA......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**(1) FARAJ ALLY SAEED**
**(2) REHEMA MWINYIJUMA – POPOTE ULIPO/MLIPO**

**JUMA SAID KADINGO** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 4/10/2023 saa 03:00 Asubuhi mbele ya **Mh. J.W. SILLAS.** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 22 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**DONAS JOACHIMU URIO** anatangaza kupotea kwa kadi za gari aina ya **DYNA na PICK UP** zenye usajili nmaba **T 242 AAK na T 263 AAN.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/MUH/1199.2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILSON EZEKIEL AWOUR** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 414 DDQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MAR/MUS/777/2023**


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**



Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.
Nipashe MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ufaransa kuwaondoa wanajeshi wake Niger

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron, ametangaza kuondoka kwa jeshi lake huko Niger, hatua inayokwenda sambamba na kumrejesha nyumbani Balozi wa Ufaransa baada ya mapinduzi ya kijeshi yaliyomuondoa Rais Mohammed Bazoum.

Tangazo hilo la siku moja iliyopita, limepokelewa vyema na viongozi wa kijeshi wa Niger wakisema ni hatua njema kuelekea uhuru wa taifa lao.

Katika mahojiano maalumu kupitia televisheni ya Ufaransa, pasipo kutoa ufafanuzi wa kina, Macron alisikika akisema Ufaransa imeamua kumuondoa Balozi wake katika kipindi cha masaa kadhaa yajayo lakini pia wanadiplomasia wake kadhaa watarejea nyumbani.

**Tulikuwa katika ardhi ya Niger kwa ombi lao, la Burkina Faso na Mali. Na operesheni ya kijeshi la Barkhane, imekuwa ya mafanikio...**

Aliongeza kuwa ushirikiano wa kijeshi kati ya mataifa hayo umekwisha na wanajeshi wa Ufaransa watajiondoa katika miezi na wiki zijazo na kujiondoa kikamilifu mwishoni mwa mwaka.

Rais Macrona alisema "Tulikuwa katika ardhi ya Niger kwa ombi lao, la Burkina Faso na Mali. Na operesheni ya kijeshi la Barkhane, imekuwa ya mafanikio kwa sababu bila ya hiyo, nchi nyingi kati ya hizi zingekuwa tayari zimechukuliwa na makundi ya wenye itikadi kali."

Aidha, ilielezwa kuwa watawala wa kijeshi wa Niger walijibu hatua hiyo kupitia taarifa iliyosomwa kwenye televisheni ya taifa, wakisema wanasherehekea hatua mpya kuelekea uhuru wa Niger, na kwamba huo ni wakati wa kihistoria, ambao unaelezea hisia za watu wa Niger.

Shirika la Usalama wa Usafiri wa Anga barani Afrika na Madagascar (ASECNA), lilisema kwenye tovuti yake kwamba watawala wa kijeshi wamepiga marufuku ndege za Ufaransa kuruka katika anga ya nchi hiyo. Ingawa haikuwa wazi ikiwa hatua hiyo ingeathiri Balozi huyo wa Ufaransa kuweza kusafiri nje ya mipaka ya taifa hilo.

Macron, alisema katika majuma na miezi ijayo, watashauriana na wahusika huko Niger kwa sababu wangependa hatua hiyo ifanyike kwa amani.

Ufaransa ina takribani wanajeshi 1,500 nchini Niger kama sehemu ya kikosi cha kupambana na wenye itikadi kali katika eneo zima la Sahel. **DW**



Wanajeshi wa Ufaransa wakiwa katika operesheni zao za kijeshi. **PICHA: MTANDAO**

## Ndayishimiye akanusha uvumi mapinduzi

**GITEGA,** Burundi

RAIS wa Burundi Evariste Ndayishimiye, amekanusha uvumi kuhusu mapinduzi nchini mwake alipokuwa ziarani katika mataifa ya kigeni kwa muda wa wiki mbili.

Kuanzia Julai 10 mwaka huu, kiongozi huyo alienda Havana, Cuba katika mkutano wa G77, China na New York kwa katika Mkutano Mkuu wa Baraza la Umoja wa Mataifa.

Ilielezwa kuwa chini ya wiki moja baada ya kuondoka kwake, tetesi zilienea kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kupinduliwa kwa serikali yake, uvumi ambao haujulikani kwamba ulitoka wapi.

Katika hotuba yake alipofika Burundi, Rais Ndayishimiye alisema: "Unaona wanasema Waburundi huacha kulima lakini hawaachi kuongea, na wanaweza kusema naweza kuzuia kufanya kazi na wote wanakaa kwenye uvumi, halafu mnakaa na kuwapiga uvumi, kisha wanaacha kufanya kazi na kufa njaa hadi kesho".

Ndayishimiye alisema kuwa uvumi huo uliletwa na wale ambao siku zote wanataka kuichafua Burundi kwa sababu wanaona ina sauti tena duniani.

Alisema "Kwa hiyo hao ndio utawakuta wakisema, kwa hiyo tufanye nini? Nitadanganya walimwengu yale ambayo huwa tunawadanganya hata kama ni uongo kwao, tuwavunje mioyo ya watu wa Burundi."

Mbali na kile kilichosemwa na Rais Ndayishimiye, Wizara ya Ulinzi na Usalama ilitoa ujumbe kwenye mtandao wa kijamii wa X kulaani uvumi huo ulioanza kuonekana baada ya wiki moja.

Aliongeza kuwa "...Ninataka kuwatia moyo kwani mkiendelea na hayo, mkisikiliza hayo kesho tutakuwa na njaa tukiendelea kukaa..."

Burundi ni mojawapo ya nchi zenye historia ya mapinduzi mengi zaidi barani Afrika, na kwamba imekumbwa na mapinduzi 11 kwa jumla. **BBC**

## Somaliland yapuuza mapendekezo ya Museveni

**HARGEISA,** Somaliland

SOMALILAND imesema haina mpango wa kufanya mazungumzo kuhusu mipango ya kujadili suala la amani, hatua inayokuja baada ya Rais wa Uganda Yoweri Museveni, kujitolea kuwa mpatanishi kati ya eneo hilo ambalo limejitenga na serikali ya shirikisho ya Somalia.

Siku chache ziliyopita, Rais Museveni, alisema amekubali kuchukua nafasi ya mratibu wa amani kati ya pande hizo mbili baada ya kukutana na mjumbe wa serikali ya Somaliland jijini Entebbe Uganda.

Wakati wa mazungumzo hayo, Rais Museveni alisema haungi mkono mpango wa eneo la Somaliland kujitenga akisema halikuwa suala bora. Katika taarifa ya Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Somaliland, ilisema mazungumzo ya aina yoyote na serikali ya Mogadishu, hayatajadili suala ya umoja bali yanapaswa kujadili namna pande hizo mbili zinaweza kusonga mbele kibinafsi.

Somaliland ilitangaza kuwa huru kutoka kwa Somalia mwaka wa 1991 na imekuwa ikitaka kutambuliwa kama nchi huru bila ya mafanikio.

Mazungumzo kati ya pande hizo mbili yamekuwa yakifanyika kwa miaka kadhaa sasa, huku suala la uongozi wa anga, uhuru wa eneo la Somaliland yakiwa mojawapo ya mambo yanayozungumziwa. **RFI**

## Wapendekeza kurefusha muhula urais Kenya

**NAIROBI,** Kenya

SENETA Samson Cherargei ambaye ni mwanachama wa muungano unaotawala nchini Kenya amependekeza kuongezwa kwa ukomo wa muhula wa urais kutoka miaka mitano hadi saba, suala lililozua hisia kali kutoka kwa upinzani.

Cherargei alisema Rais William Ruto, ambaye amekuwa ofisini kwa takribani mwaka mmoja sasa, huenda akakosa muda wa kutosha kutekeleza manifesto yake ya kampeni.

Ilielezwa kuwa pendekezo hilo limezua hisia kali miongoni mwa baadhi ya Wakenya huku upinzani ukishutumu serikali kwa kupanga njama ya kuondoa ukomo wa mihula ya urais.

Baadha ya watumiaji wa mtandao X ambao majina yao hayakubainishwa walisema "Inafaa kwa kweli ipunguzwe hadi miaka minne kila muhula. Hii ndiyo njia pekee ya uhakika ya kuleta uwiano wa kitaifa na kuzuia maslahi binafsi kujikita wenyewe, hivyo kuruhusu utii wa katiba kutekelezwa kikamilifu," alisema.

Mwingine alisema "Iwapo kiongozi yeyote hawezi kutekeleza manifesto yake katika kipindi cha miaka 10, kuna haja gani ya kuongeza minne zaidi," alihoji. **BBC**

# TWIGA STARS YAPANIA KUPINDUA MATOKEO KWA IVORY COAST LEO

**Na Saada Akida**

TIMU ya soka ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania (Twiga Stars) leo inashuka dimbani katika mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wanawake(WAFCON) dhidi ya Ivory Coast.

**Katika mchezo wa kwanza Twiga Stars ilipoteza ugenini kwa kukubali kichapo cha mabao 2-0 mbele ya wapinzani wao hao mechi iliyopigwa Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa Charles Konan Banny uliopo Yamoussoukro, Ivory Coast.**

Katika mechi hiyo ya marudiano inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, Twiga Stars inatakiwa kushinda kuanzia mabao 3-0 ili kusonga mbele.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, ameongeza nguvu kwenye kikosi chake baada ya kuwajumuisha nyota wawili akiwamo Judith Singano na Clara Luvanga kwa ajili ya kusaka ushindi huo muhimu.

Kuelekea mchezo wa leo, Shime amesema wamejiandaa vizuri kwa mechi hiyo ya pili wanayotakiwa kupata ushindi kuanzia mabao 3-0 ili kutoa Ivory Coast katika mbio hizo za kufuzu.

Alisema baada ya kupoteza kwa mabao 2-0 ugenini na kurejea nyumbani kufanya maandalizi mazuri, anaamini mechi ya leo ina uhai kwao kuweza kufanya vizuri.

"Kuna wachezaji tumewaongeza akiwamo Singano na Clara, haileti maana mechi ya kwanza kutakuwapo kwao ndiko kumesababisha kupoteza ila kuwapo kwenye mechi hii wataongeza kitu ndani ya kikosi.

"Tunaenda kucheza na timu bora, kwa viwango wako juu lakini hatutaingia kinyonge kwa sababu tuna uwezo wa kuwafunga ila kazi kubwa ni kuwatoa mashindanoni jambo ambalo linawezekana," alisema Shime.

Alisisitiza kuwa sasa wanawafahamu wapinzani wao vizuri na wapi wanaweza kuwazuia wasiwafunge, lakini wapite njia gani ili kufanikiwa kushinda idadi ya mabao 3-0 na kuwatoa katika mbio hizo za kuwania tiketi ya kufuzu WAFCON.

"Niwaombe Watanzania wajitokeze kwa wingi kwa sababu nguvu yao inatakiwa iwepo, kuja kusapoti timu siku ya kesho (leo)," alisema kocha huyo.

Kwa niaba ya wachezaji wa Twiga Stars, Anastazia Katunzi, alisema wamejipanga vizuri kwa mchezo wa leo na kwa matokeo ya kupoteza mechi ya kwanza hawataingia kinyonge na wanashuka dimbani kwa kuhakikisha wanawatoa Ivory Coast.

"Hatutakuwa wanyonge, bado hatujakata tamaa kisa eti tumepoteza mechi ya kwanza, kocha Shime amefanyia kazi makosa yaliyojitokeza mechi iliyopita na tunaenda kuwaondoa Ivory Coast na kutafuta tiketi ya kufuzu," alisema Nastazia.

Naye Kocha wa Ivory Coast, Toure Clement, alisema wamefanya maandalizi mazuri na kazi kubwa iliyopo kwa wachezaji wake ni kwenda kufanya majukumu yao ya kutafuta ushindi na anaimani bahati itakuwa kwao na kupata matokeo mazuri.

"Licha ya kupata matokeo nyumbani ni tofauti na mechi ya kesho (leo), tunasahau matokeo hayo na tunaanza upya kwa mchezo wetu huu wa marudiano dhidi ya Tanzania," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa Tanzania ina timu nzuri na wanaiheshimu kwa sababu wana wachezaji wazuri kwa mmoja mmoja na anaimani hapo mbele itakuwa tishio.



Mwenyekiti wa Kamati ya Olympiki Tanzania, Henry Tandau (kushoto), akimkabidhi fulana za Olympiki Tanzania, Balozi wa Urusi hapa nchini, Andrey Avetisyan, katika kongamano la kuwajengea uwezo vijana wa Kitanzania lililofanyika jijini Dar es Salaam jana na kuwapa mrejesho wa kongamano lililofanyika nchini Urusi na kuwakutanisha vijana wa Afrika hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Ruvu Shooting taabani Championship*

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu ya Polisi Tanzania ikichapwa bao 1-0 juzi dhidi ya Green Warriors kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, timu ya Ruvu Shooting imepoteza mechi zake zote tatu za Ligi ya Championship mpaka sasa.

Timu hizo zote mbili zilikuwa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ziliteremka moja kwa moja msimu uliokwisha.

Polisi Tanzania imepoteza mechi yake ya kwanza kwenye raundi ya tatu na sasa inashika nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi inayoongozwa na Mbeya Kwanza.

Timu ya Ruvu Shooting inaburuza mkia baada ya Jumamosi kupoteza mechi yake kwa mabao 3-0 dhidi ya KenGold.

Kabla ya kapo ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania na mechi ya ufunguzi wa ligi hiyo ilinyooshwa mabao 2-1 dhidi ya FGA Talent, hivyo haina pointi yoyote mpaka sasa.

Mechi nyingine iliyochezwa juzi Jumapili ni kati ya Biashara United dhidi ya Copco, katika Uwanja wa Karume, Musoma, mkoani Mara, wenyeji wakishinda mabao 2-0 yaliyofungwa na Herbert Charles na Isaya Kuzoza, huku Transit Camp ikiidungua FGA Talents bao 1-0 Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, likiwekwa kwenye kamba na Rashid Silla.

Msimamo wa ligi hiyo unaonyesha kuwa Mbeya Kwanza ipo juu kwa pointi saba na mabao saba, KenGold ya pili pointi saba mabao matano na Mbuni pointi saba mabao matano, lakini imefungwa mabao mengi.

## Lipumba mgeni rasmi bonanza la michezo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi nchini (CUF), Seif Lipumba, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika bonanza la michezo mbalimbali, litilopangwa kufanyika Oktoba 3, mwaka huu katika viwanja vya Kisese Bisa vilivyopo Kondoa mkoani Dodoma.

Bonanza hilo la michezo limeandaliwa na CUF Kata ya Kisese, ambapo timu za michezo mbalimbali kutoka katika kata tofauti zinatarajiwa kushiriki.

Lengo la bonanza hilo ni pamoja na kusapoti jitihada za serikali katika kukuza vipaji vya wachezaji kuanzia ngazi ya chini hadi taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Makamu Mwenyekiti wa CUF Kata ya Kisese, Salum Abdalah, alisema katika bonanza hilo kutakuwa na michezo mbalimbali ambayo itashindaniwa, ikiwamo soka, netiboli, kuvuta kamba, kufukuza kuku pamoja na mpira wa wavu kwa timu za wanawake na wanaume ambazo zinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na bonanza hilo.

"Pamoja na kufanya siasa, lakini Chama cha CUF kinatambua umuhimu wa michezo, ndio maana tumeandaa bonanza hilo," alisema Sudi.

## Kocha Zimamoto atoa sababu sare

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Timu ya Zimamoto, Mohmed Hilali, amesema matokeo ya sare waliyopata katika michezo miwili ya Ligi Kuu Zanzibar yametoka na wachezaji wake wengi kuandamwa na majeruhi.

Zimamoto FC juzi ilipata tena sare ya pili katika mchezo dhidi ya Mafunzo SC, uliopigwa kwenye Dimba la Mau A majira ya saa kumi alasiri na kumalizika timu hiyo kufungana bao 1-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto FC, Hilali, alisema jumla ya wachezaji watano wa kikosi cha kwanza ni majeruhi, hali iliyochangia kutokuwapo katika mechi hizo na walikuwa na nafuu na kucheza hawakumaliza dakika zote 90.

Alisema katika mchezo huo dhidi ya Mafunzo ilimlazimu kufanya mabadiliko ya wachezaji hao kutokana na hali zao na ndicho kilichochangia kushindwa kupata ushindi.

"Majeraha ya wachezaji wangu tegemezi ndio iliyopelekea tushindwe kufanya vizuri katika mchezo huu, mchezo wa kwanza sikutambua mapema ila mchezo huu ndio nimetambua kama wachezaji hawapo sawa, lakini hawasemi hali iliyonifanya kipindi cha pili kufanya mabadiliko nisiyoyategemea," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

### ONANA KUMPISHA OBLAK

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua mlinda mlango wa Atletico Madrid raia wa Slovenia, Jan Oblak, 30, ikiwa wataamua kumwonesha Mcameroon Andre Onana, 27, mlango wa kutokea baada ya kuanza maisha vibaya pale Old Trafford. ***(Fichajes)***

### WHARTON AWANIWA UNITED

EVERTON na Manchester United ni miongoni mwa klabu zinazofuatilia maendeleo ya kiungo wa kati wa Blackburn, Adam Wharton, 19. ***(Alan Nixon via Teamtalk)***

### LIVER KUMUUZA ALCANTARA

LIVERPOOL itakuwa tayari kukubali ofa kubwa kwa kiungo wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara, 32, katika dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### NYOTA WAPYA ENGLAND

NAFASI za baadhi ya wachezaji wa Arsenal zinaweza kuwa hatarini huku viungo wa kati wa England, Ethan Nwaneri na Myles Lewis-Skelly wakitarajiwa kuingia katika kikosi cha kwanza katika miaka miwili ijayo. ***(Express)***

### TONEY KUSEPA BRENTFORD

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Ivan Toney, 27, yuko tayari kuondoka Brentford Januari na klabu hiyo iko tayari kumwachia mchezaji huyo ambaye anatumikia marufuku ya miezi nane kwa kukiuka sheria za kamari za FA. ***(The Mirror)***

### ARNOLD MKATABA MPYA

BEKI wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold, 24, amejitolea kikamilifu kwa kikosi cha Liverpool na anakaribia kusaini mkataba mpya. ***(Football Insider)***

### FERGUSON NA BRIGHTON

MSHAMBULIAJI wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, aliamua kusalia na 'Seagulls' hao ni bora kwa maendeleo yake kuliko kuhamia Manchester United baada ya klabu hiyo kuonesha nia ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 msimu wa majira ya joto. ***(The Mirror)***

### RASHFORD, POGBA WALIKATAA

MARCUS Rashford na Paul Pogba walikuwa wachezaji wa Manchester United ambao walikataa nafasi ya kuwa nahodha wa klabu hiyo chini ya Ole Gunnar Solskjaer. ***(The Sun)***

### RODRYGO ASAKWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inavutiwa na winga wa Real Madrid na Brazil, Rodrygo, 22, ili kukabiliana na miamba hiyo ya Hispania inayomsaka fowadi wao wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 24. ***(Football Transfers)***


### DAVIES AWANIWA MADRDID

REAL Madrid pia wana nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 22, kutoka Bayern Munich. ***(Football Transfers)***

### YOUNG ANYATIWA CITY

KLABU ya Manchester City imeelekeza macho yake kwa mlinda mlango wa Sunderland, Matty Young, 16. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTI ATOA SABABU KICHAPO REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

● ● ● Tulikuwa tete, haukuwa usiku mzuri kwenye safu ya ulinzi, ilikuwa dhaifu na...

CARLO Ancelotti amelaumu "udhaifu wa safu ya ulinzi" wakati Real Madrid ikichapwa mabao 3-1 kwenye mchezo wa dabi dhidi ya Atletico Madrid katika Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumapili.

**Pamoja na kulaumu safu yake ya ulinzi, lakini alikataa kukosoa mchezaji mmoja mmoja, akisema kupoteza ni "kosa langu."**

Alvaro Morata aliiweka Atletico mbele baada ya dakika nne pekee kwenye Uwanja wa Metropolitano, kabla ya Antoine Griezmann kufanya matokeo kuwa 2-0.

Toni Kroos aliifungia Real Madrid bao, lakini bao la kichwa la Morata baada ya mapumziko liliwahakikishia Atletico pointi tatu.

Matokeo hayo yanawaacha Real Madrid wakiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo na pointi zao 15 - moja nyuma ya Barcelona na Girona - huku Atletico wakiwa na pointi 10 na mchezo mmoja mkononi.

"Tatizo lilikuwa udhaifu wa ulinzi," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi. "Katika mechi sita msimu huu tulikuwa tumefungwa mabao matatu, na leo (juzi) tumeruhusu matatu ndani ya dakika 45.

"Tulikuwa tete, haukuwa usiku mzuri kwenye safu ya ulinzi. Sitaingia kwa mtu mmoja mmoja, lakini hatukulinda vizuri. Hatukuwa na nafasi nzuri.

Huku Vinicius Junior akikosekana kwenye kikosi cha Real Madrid kutokana na kuchelewa kupona majeraha, Ancelotti aliamua kumchezesha Jude Bellingham kama fowadi pamoja na Rodrygo huku Luka Modric na Toni Kroos wote wakianza katika safu ya kati kwa mara ya kwanza msimu huu.

"Mfumo haukubadilika," alisema Ancelotti.

"Tulianza na Modric kama namba 10 na washambuliaji wawili, Bellingham na Rodrygo. Labda ningefanya vizuri zaidi, wakati timu haifanyi kile ambacho ingeweza kufanya, ni wazi kwamba hilo ni jukumu langu.

Kocha wa Atletico, Diego Simeone, alisifu kiwango cha timu yake na Morata, ambaye sasa amefunga mabao matano kwenye LaLiga.

"Alvaro alicheza mchezo wa kuvutia," alisema Simeone. "Tunamhitaji Morata huyu. Tunajua anaweza kufanya hivyo. Tunajua ana zana za kupata. Tutegemee anaweza kudumisha kiwango hiki, kwa sababu kwa Hispania na Atletico Madrid ni fowadi muhimu.

"Nina furaha sana kwa mashabiki, Morata alisema. Hali ya hamasa ilikuwa ya ajabu. Sote tulikuwa pamoja, sisi uwanjani na wao kwenye majukwa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 718,3

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
CRYSTAL PALACE
1 | 1.59
X | 3.96
2 | 4.91

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ‘WACHEZAJI CHELSEA WANAHITAJI KUKUA’




**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino, amesema wachezaji wake wa Chelsea wanahitaji kukua kama timu baada ya kuchapwa bao 1-0 na Aston Villa kwenye Uwanja wa Stamford Bridge na hivyo kupoteza kwa mara ya tatu msimu huu.

Mchezo uligeuka baada ya kutolewa nje kwa Malo Gusto wa Chelsea baada ya dakika 58. Lucas Digne alichezewa rafu kwenye kifundo cha mguu na baada ya ukaguzi wa VAR mwamuzi Jarred Gillett, alibadilisha kadi ya njano ya awali na kuwa nyekundu kwa mchezo hatari.

Pochettino alimuingiza Ben Chilwell na kumsogeza Axel Disasi kuwa beki wa kulia, lakini hakukuwa na matokeo chanya kwa Chelsea. Ulikuwa uamuzi ambao uliwasumbua, kwani kwa upande wa wenyeji walijidhatiti na Moussa Diaby alimtengenezea pasi Ollie Watkins, ambaye alifunga bao.

Baada ya mchezo huo, Pochettino alisema wachezaji wake wanatakiwa kukua kama wachezaji na wanapaswa kuchukua hatua baada ya mwanzo mbaya wa timu msimu huu.

“Ni jukumu letu na jukumu la wachezaji,” alisema Pochettino.

“Hatuwezi kulaumu VAR au mwamuzi. Tunatakiwa tufanye tofauti kwa namna tofauti. Sitalaumu wala kusema lolote dhidi ya Malo Gusto. Hali hutokea kwenye soka na huathiri mchezo na timu kwa njia hasi.

“Tunahitaji kukua kama timu, si tu kwa njia ya kibinafsi.”



## Klopp amsifia Nunez kuimarik

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amefichua kuwa “tofauti kuu” kwenye mchezo wa Darwin Nunez msimu huu ni kiwango chake.

Nunez alisajiliwa kwa kitita cha pauni milioni 65 na Liverpool kutoka Benfica msimu uliopita wa majira ya joto, lakini alikuwa ndani na nje ya kikosi cha kwanza katika kipindi chote cha msimu akicheza katika mechi 19 kati ya 29 za Ligi Kuu.

Licha ya hayo na kusajiliwa kwa Cody Gakpo - mchezaji ambaye alionesha kiwango cha juu katika kipindi cha pili cha msimu uliopita - Liverpool walionesha imani kwa Nunez kama mshambuliaji wao wakati wa majira ya joto kwa kumpa raia huyo wa Uruguay jezi namba tisa.

Na tangu wakati huo, Nunez amelipa zaidi ya imani iliyooneshwa kwake. Raia huyo wa Uruguay amefikisha mabao manne kufikia sasa msimu huu wa 2023/24, huku bao lake la hivi majuzi likiwa ni katika ushindi wa 3-1 dhidi ya West Ham United kwenye Uwanja wa Anfield.

“Hatua kubwa katika wiki chache zilizopita. Yeye ni tishio. Nyote mliona bao, labda lilikuwa zuri sana, sivyo? ilikuwa kali sana. Ali akipatikana kwetu kila wa ni muhimu sana kwetu k ba tunaye - sina uhaki neno sahihi kwake.

“Piga mpira hapo, u kifuani na ucheze ku hapo, kama vile tulifun tatu kwa Wolves. Na hiyo ilikuwa hali kama hi muhimu sana kwetu.

“Kazi ya ulinzi anayo sasa, labda ndiyo tofauti Siku zote alitaka, lakini ili chini ya uratibu. Sasa hiy onekana bora zaidi na tu njia ya jinsi ya kuifanya k naye.”



345,550

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 27/09/2023 | 21:30 | St. Gallen vs BSC Young Boys | 2.55 | 3.50 | 2.26 |
| 2. 27/09/2023 | 21:30 | Catanzaro vs Cittadella | 2.22 | 3.13 | 3.13 |
| 3. 27/09/2023 | 21:30 | Como vs Sampdoria | 2.71 | 3.12 | 2.49 |
| 4. 27/09/2023 | 21:45 | Chelsea vs Brighton | 2.20 | 3.43 | 2.95 |
| 5. 27/09/2023 | 21:45 | Royal Antwerp vs KAA Gent | 2.23 | 3.45 | 2.95 |
| 6. 27/09/2023 | 22:00 | Newcastle vs Manchester City | 2.95 | 3.43 | 2.20 |
| 7. 27/09/2023 | 22:30 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.52 | 3.14 | 2.99 |
| 8. 27/09/2023 | 22:30 | Valencia vs Real Sociedad | 2.46 | 3.08 | 3.13 |
| 9. 28/09/2023 | 19:00 | Ismaily SC vs El Ittihad Alexandria | 2.37 | 3.09 | 2.94 |
| 10. 28/09/2023 | 19:30 | Monza vs Bologna | 2.41 | 3.34 | 2.98 |
| 11. 28/09/2023 | 20:00 | Granada vs Betis | 2.85 | 3.36 | 2.49 |
| 12. 28/09/2023 | 20:00 | Orebro SK vs Utsiktens BK | 2.39 | 3.30 | 2.88 |
| 13. 28/09/2023 | 22:30 | Osasuna vs Atletico Madrid | 3.19 | 3.45 | 2.24 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 26/09/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2114 | Rukh Vinnyky vs Oleksandria | 2.28 | 2.95 | 3.10 |
| 16:00 | 2301 | FK Radnicki 1923 vs Radnik Surduluca | 2.03 | 3.00 | 3.40 |
| 17:00 | 2352 | Veres Rivne vs Shakhtar Donetsk | 8.95 | 5.29 | 1.25 |
| 18:00 | 1325 | Radnicki Nis vs FK Zeleznicar Pancevo | 1.68 | 3.50 | 4.20 |
| 18:45 | 4697 | Italy W vs Sweden W | 2.96 | 3.37 | 2.15 |
| 19:00 | 2383 | Coca Cola vs El Daklyeh | 1.76 | 3.42 | 4.47 |
| 19:15 | 1354 | Germany W vs Iceland W | 1.23 | 5.30 | 9.99 |
| 19:15 | 3281 | Calcio Lecco vs Feralpisalo | 2.49 | 3.04 | 2.78 |
| 19:15 | 5596 | Cosenza vs Cremonese | 2.97 | 3.02 | 2.37 |
| 19:30 | 3544 | Austria W vs France W | 7.53 | 4.38 | 1.35 |
| 20:00 | 1036 | Sevilla FC vs Almeria | 1.58 | 4.21 | 5.55 |
| 20:00 | 1356 | Istanbulspor vs Galatasaray | 5.81 | 4.56 | 1.44 |
| 20:15 | 2509 | Portugal W vs Norway W | 2.95 | 3.40 | 2.14 |
| 20:30 | 1818 | Neuchatel Xamax vs FC Baden | 1.41 | 4.44 | 5.65 |
| 20:30 | 2530 | Stade Nyonnais vs FC Wil | 2.68 | 3.49 | 2.22 |
| 20:30 | 5004 | FC Schaffhausen vs AC Bellinzona | 1.99 | 3.63 | 3.02 |
| 20:30 | 5288 | Hapoel Tel Aviv vs Maccabi Tel Aviv | 5.66 | 4.14 | 1.45 |
| 20:30 | 5726 | Chippa Utd vs SuperSport Utd | 3.30 | 2.68 | 2.41 |
| 21:00 | 2745 | Netherlands W vs England W | 2.90 | 3.31 | 2.21 |
| 21:30 | 2741 | Sudtirol vs Modena | 2.72 | 2.93 | 2.62 |
| 21:30 | 3401 | AC Reggiana vs Pisa | 2.61 | 3.08 | 2.61 |
| 21:30 | 5366 | Ascoli vs Ternana | 2.31 | 3.18 | 2.92 |
| 21:30 | 5452 | Venezia vs Palermo | 2.26 | 3.19 | 2.99 |
| 21:30 | 5641 | FC Zurich vs Grasshoppers | 1.66 | 3.87 | 4.44 |
| 21:30 | 5874 | Spezia vs Brescia | 1.84 | 3.33 | 4.05 |
| 21:45 | 1299 | Ipswich vs Wolverhampton | 2.70 | 3.45 | 2.36 |
| 21:45 | 1548 | Exeter vs Luton Town | 4.28 | 3.69 | 1.72 |
| 21:45 | 1740 | US Quevilly Rouen vs Angers | 2.68 | 3.18 | 2.48 |
| 21:45 | 1801 | Juventus vs Lecce | 1.62 | 3.85 | 5.84 |
| 21:45 | 1887 | Bradford City vs Middlesbrough | 4.17 | 3.67 | 1.75 |
| 21:45 | 2749 | Caen vs Grenoble Foot | 1.85 | 3.37 | 3.96 |
| 21:45 | 3143 | Guingamp vs Bordeaux | 2.66 | 3.16 | 2.51 |
| 21:45 | 3311 | Rodez Aveyron vs Troyes | 1.89 | 3.47 | 3.66 |
| 21:45 | 3349 | Salford City vs Burnley | 6.36 | 4.27 | 1.44 |
| 21:45 | 4139 | Preussen Munster vs Bayern Munchen | 20.99 | 8.22 | 1.12 |
| 21:45 | 4414 | Bastia vs PAU FC | 1.74 | 3.57 | 4.27 |
| 21:45 | 4946 | Amiens vs AC Ajaccio | 2.13 | 3.12 | 3.32 |
| 21:45 | 5049 | Port Vale vs Sutton United | 1.66 | 3.78 | 4.58 |
| 21:45 | 5248 | Scotland W vs Belgium W | 2.23 | 3.41 | 2.80 |
| 21:45 | 5356 | Cliftonville Belfast vs Coleraine FC | 1.75 | 3.59 | 3.84 |
| 21:45 | 5651 | Paris FC vs Laval | 2.68 | 3.03 | 2.58 |
| 21:45 | 5722 | AJ Auxerre vs Annecy FC | 1.53 | 3.92 | 5.55 |
| 21:45 | 5744 | Valenciennes vs Concarneau | 2.17 | 3.18 | 3.18 |
| 21:45 | 5773 | Kilmarnock vs Hearts | 2.70 | 3.00 | 2.52 |
| 21:45 | 5849 | Mansfield vs Peterborough | 2.24 | 3.43 | 2.88 |
| 22:00 | 1421 | Lille vs Reims | 1.95 | 3.80 | 3.65 |
| 22:00 | 4437 | Manchester Utd vs Crystal Palace | 1.59 | 3.96 | 4.91 |
| 22:00 | 5911 | Spain W vs Switzerland W | 1.14 | 6.52 | 14.26 |
| 22:30 | 4184 | Mallorca vs Barcelona | 5.47 | 3.90 | 1.64 |
| 23:30 | 2874 | Universitario Popayan vs Club Cortulua | 2.00 | 3.31 | 3.36 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WANAMUZIKI 200 KUTUMBUIZA TAMASHA LA MARAFIKI NCHINI

**Na Moshi Lusonzo**

JUMLA ya wasanii 200 wa muziki kutoka mataifa mbalimbali watatumbuiza katika Tamasha la Kimataifa la Muziki la Marafiki, litakalofanyika Oktoba mwaka huu jijini Dar es Salaam na Bagamoyo mkoani Pwani.

Akizungumza katika uzinduzi wa tanasha hilo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Asedeva, Isack Abeneke, alisema tamasha hilo la siku nne litafanyika katika sehemu mbili hapa nchini, jijini Dar es Salaam na Bagamoyo mkoani Pwani kuanzia Oktoba 5 hadi 7, mwaka huu.

**Alisema tamasha hilo lililoandaliwa kwa kushirikiana na Ubalozi wa Ufaransa nchini chini ya mpango wa Sanaa Pro, litahusisha burudani ya muziki wa jukwaani na mafunzo kwa wanamuziki watakaohudhuria.**

"Kutakuwa na majukwaa mawili ya muziki, moja litakuwa Makumbusho, Dar es Salaam kwa siku tatu na Bagamoyo mkoani Pwani kwa siku moja. Tumefanya hivi ili wasanii wetu waweze kutoa burudani kamili na watu wengi wahudhurie," alisema Abebeke.

Alisema wasanii walioothibitisha kushiriki ni kutoka Tanzania, Ufaransa, Afrika Kusini na visiwa vya Reunion'.

Aliwataja baadhi ya wasanii wa hapa nchini watakaopanda jukwaani kuwa ni Amini, Dula Makabila na Baba Kush.

"Katika kutimiza malengo yao tutatoa mafunzo kwa siku zote nne namna ya wasanii kukitambua na kuthamini muziki kama urithi wao, jinsi ya kutumia mitandao ya kijamii kujiinua kiuchumi na kujua umuhimu wa hakimiliki ya kazi zao," alieleza.

Etienne Pellausy kutoka Idara ya Utamaduni ya Ubalozi wa Ufaransa, alisema wameamua kuunga mkono tamasha hilo kutokana na umuhimu wake katika kulitambulisha taifa nje ya mipaka.

Alisema nchi yake inatambua utamaduni ni kama alama ya umoja na mshikamano katika jamii na ndio maana wasanii kutoka katika nchi hiyo watahudhuria.

## Yanga yataja jeuri yao

INATOKA UK. 24

hiyo baada ya hapo, niwasihi tu wanachama na mashabiki wa Yanga kujitokea kwa wingi kuwapa morali wachezaji wetu kuhakikisha wanakamilisha ile kazi ambayo tumewatuma, kama tulikuwa kwa wingi kule Kigali, Rwanda, basi tunaoneshe kuwa hapa ni nyumbani," alisema Arafat.

Yanga ina matumaini makubwa ya kutinga makundi kutokana na kumiliki kwa kiasi kikubwa mechi ya kwanza nchini Rwanda, huku wapinzani wao wakionekana kupaki basi zaidi kuliko kushambulia.

Al-Merrikh ilicheza nchini Rwanda badala ya Sudan kutokana machafuko makubwa ya kisiasa nchini mwao ambapo kwa kiasi kikubwa imeziathiri timu za nchini humo kwani zimekuwa dhaifu kutokana na kutowapo kwa ligi, lakini pia wachezaji wao wengi wa kigeni kuamua kuondoka kwa kuvunja mikataba yao.

Yanga ambayo msimu uliopita ilicheza fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, inahitaji ushindi wowote katika mechi hiyo ya Jumamosi, sare yoyote au isifungwe mabao yanayoanzia mawili ili kutinga makundi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 24 kupita.

TENISI...



Mchezaji wa Tenisi, Omari Abdallah, akipiga mpira kurudisha kwa mpinzani wake (hayupo pichani), wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na michuano ya mchezo huo inayotarajiwa kufanyika jijini Arusha mwezi ujao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Michezo

Jumanne Septemba 26, 2023

Nipashe




Klopp amsifia Nunez kuimarika UKURASA 22

# Robertinho amjaza 'madini' Kennedy kuiva na Malone

●●● Kuwapa mechi ya kirafiki leo ili kupata muunganiko, asema lengo ni Dynamos ife...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwa na uhakika wa kumkosa Henock Inonga 'Varane', katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, ameanza kumpa 'madini' tangia kuanza kwa msimu huu, Inonga, amekuwa akiongoza safu ya ulinzi ya Simba kwa kushirikiana vema na Mcameroon Fondon Che Malone, ambaye amerithi viatu vya Joash Onyango aliyetimkia Singida Fountain Gate FC.

**Lakini wiki iliyopita katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union, Inonga alipata majeraha ya mguu wa kulia baada ya kuchezewa rafu mbaya na Haji Ugando, hivyo hatokuwa sehemu ya kikosi kitakachoivaa Power Daynamos Jumapili wiki hii kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.**

Kwa kulitambua hilo, Robertinho, ambaye ana kazi kubwa ya kuhakikisha Simba inapata matokeo ya jumla ili kutinga hatua ya makundi baada ya timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2 kwenye mchezo wa kwanza nchini Zambia, ameanza kumpika vilivyo Kennedy ili kupata muunganiko mzuri na Malone.

Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema kwa sasa ameanza mchakato wa kumjenga Kennedy kuelekea mchezo huo kutokana na kumkosa Inonga.

"Tunaendelea kuweka mikakati na mipango yetu sawa katika uwanja wa mazoezi kuelekea katika mchezo wetu muhimu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kutokana na matokeo ya mchezo wetu wa kwanza tuliocheza Zambia, nimeanza kumtengeneza Juma [Kennedy] ili aweze kucheza kati na Che Malone, naamini atafanya vizuri kwa sababu si mara ya kwanza, amefanya hivyo katika mechi za Ngao ya Jamii mpaka tukaibeba.

"Nimeamza kumuweka sawa kulingana na presha ya mchezo wenyewe pamoja na kuongea naye kila mara ili kuwa kwenye kiwango bora cha kuweza kupata matokeo," alisema Robertinho.

Alisema anaimani kikosi chake kitafanya vizuri kwa sababu wameanza mazoezi kuelekea mchezo wao wa marudiano dhidi ya Power Dynamos lengo likiwa ni kupata ushindi na kufuzu hatua ya makundi.

Inonga ambaye aliumia katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na kushonwa nyuzi 13 katika mchezo huo wa Ligi Kuu Bara, ambao Simba iliondoka na ushindi wa mabao 3-0, imeelezwa pia ataukosa mchezo ujao wa ligi hiyo ugenini dhidi ya Tanzania Prisons.

Simba inahitaji kupata ushindi wowote, suluhu ama sare ya bao 1-1, ili kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, matokeo ambayo wakiyapata watakuwa katika mwendo mzuri wa kuelekea kutimiza malengo yao kucheza nusu fainali ya michuano hiyo msimu huu.

Hata hivyo, katika kuhakikisha wachezaji wake wanakuwa imara na safu yake hiyo ya ulinzi inapata muunganiko mzuri, Robertinho ameomba mechi ya kirafiki ambapo Simba itacheza leo dhidi ya Pan African, utakaopigwa Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju, saa 3:00 asubuhi.

Aliongeza kuwa anaimani kubwa na mechi hiyo ya kirafiki ambayo wanacheza, kumsaidia kuona kile alichowaelekeza wachezaji kimefanyiwa kazi kabla ya mchezo dhidi ya Power Dynamos.



Kocha Msaidizi wa Simba, Mtunisia Ouanane Sellami, akimwongoza beki wa timu hiyo, Che Malone wakati wa mazoezi. Timu hiyo itaikaribisha Power Dynamos Jumapili katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kwenye mechi ya mkondo wa pili ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yataja jeuri yao kwa Al Merrikh

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema haina shaka na mechi ya Ligi ya Mabingwa itakayochezwa Jumamosi ijayo dhidi ya Al Merrikh ya Sudan kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ikitamba kuwa itamalizia ilipoishia.

Makamu wa Rais wa klabu hiyo, Arafat Haji, amesema ushindi wa mabao 2-0 ugenini katika Uwanja wa Kigali Pele, Nyamirambo nchini Rwanda, uliochezwa Septemba 16, mwaka huu, unawapa matumaini makubwa ya kutinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza tangu 1998.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Arafat alisema kingine ni ubora wa Kocha wao Mkuu, Miguel Gamondi na kikosi chao pia unawapa jeuri ya kutimiza malengo yao ya awali ya kutinga hatua hiyo.

"Tunajua mchezo haujamalizika, dakika 90 za mchezo wa kwanza zimekwisha pale Kigali, Rwanda na Mungu akatujaalia tukapata ushindi wa mabao 2-0 ugenini, lakini kwa kuiangalia timu yetu, maandalizi ya mwalimu Miguel Gamondi, na ubora wa kikosi chetu, basi ni matumaini yetu kuwa tunakwenda kukamilisha pale palipobakia na kusonga hatua inayofuata ya makundi," alisema kiongozi huyo.

Alisema watakapofanikiwa kutinga hatua hiyo, hatua inayofuata itakuwa ni kujipanga wao kama uongozi na kuangalia jinsi gani watavyocheza hatua hiyo na lengo lao litakuwa kufika mbali.

"Kwa awamu hii ya kwanza hatua yetu ni kufuzu kutinga makundi na tukishafika huko tutajipanga ili kuona tunafika mbali kwenye michuano

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >